# NJIA YA UTENDAJI

SURA YA KWANZA

# NJIA YA KUTAKATA

## I
## UTAKASO WA MOYO

1. Watu wana tamaa za kidunia ambazo huwaingiza katika mateso na madanganyo. Zifuatazo ni njia tano za kujikomboa kutokana na minyororo ya tamaa za dunia.

Kwanza hawana budi kuwa na mawazo sahihi juu ya mambo; mawazo yanayotokana na uchunguzi wa makini, na kuelewa sababu na matokeo au madhara yake na kutambua umuhimu wake. Kwa kuwa chanzo na sababu za mateso vipo ndani ya tamaa za moyo na shauku na kwa kuwa tamaa na shauku vinahusiana katika kupotosha mtazamo wa nafsi ya mtu bila kujali sheria ya chanzo na matokeo, na kwa sababu inatokana na mtizamo potofu, imani itapatikana tu moyo utakapoondokana na tamaa hizi za kidunia.

Pili, watu wanaweza kuondokana na mtazamo potofu na matokeo yake ya tamaa za kidunia kwa kuutawala moyo kwa utararibu na uangalifu. Kwa kuutawala moyo kwa utaratibu na uangalifu wanaweza kuepukana na tamaa zitokanazo kwa kuchochewa na macho, masikio, pua, ulimi, ngozi na taratibu nyingine za akili kama hizo na kwa kufanya hivyo, watu wanaikata mizizi inayochipua tamaa zote za kidunia.

Tatu, yawapasa kuwa na mawazo sahihi kuhusu matumizi ya vitu vyote. Hii ina maana kuwa, kuhusu chakula na mavazi, wasivifikirie katika upande wa raha na starehe ila katika mahitaji ya mwili. Mavazi ni ya lazima katika kuukinga mwili kutokana na baridi, au joto kali au kuusitiri aibu zake; chakula ni muhimu na lazima kuulisha mwili wakati mwili huo unapokea Uongofu na U-Buddha. Tamaa za dunia haziwezi kujitokeza katika fikra za namna hiyo.

Nne, watu yawapasa kujifunza uvumilivu; lazima wajifunze kuvumilia adha ya joto na baridi; kiu na njaa; lazima wajifunze kuwa wastahimilivu wanapopokea bezo na matusi; kwa vile tendo la kukubali uvumilivu ndilo lizimalo moto wa tamaa za kidunia unaounguza miili yao.

Tano, ili watu waepuke hatari lazima wajifunze kuona. Kama mtu mwenye hekima anavyokaa mbali na farasi pori au mbwa kichaa, vivyo hivyo yampasa mtu asiwe na marafiki waovu au kwenda kwenye sehemu zinazokwepwa na watu wenye busara. Ikiwa mtu atajenga na kushika tabia ya tahadhari na busara, moto wa tamaa za kidunia unaowaka katika viungo vya mwili wake utazimika.

2. Kuna makundi matano ya tamaa duniani. Tamaa zinazotokana na sura na maumbo yaonekanayo machoni; zinazotokana na sauti zisikiwazo na masikio, zinazotokana na harufu nzuri inuswayo na pua; zinazotokana na maonjo ya ulimi; zinazotokana na vitu vinavyokubalika kwa njia ya mguso.

**Njia ya kutakata**

Kutokana na milango hii mitano ya tamaa tunapata upendo wa faraja ya mwili.

Watu wengi wanaposhawishiwa na upendo wa faraja ya mwili, hawagundui maovu yanayoambatana na faraja na hukamatwa katika mitego ya ibilisi kama mnyama akamatwavyo na mtego msituni. Kwa hakika, milango hii mitano ya tamaa ni mitego ya hatari hasa. Watu wakamatwapo katika mitego hii huangaika katika maumivu na mateso ya kidunia. Yawapasa kutambua namna ya kuepukana na mitego hiyo.

3. Hakuna njia ya kuepuka mateso ya kidunia. Fikiria ukimkamata nyoka, mamba, ndege, mbwa, mbweha na nyani, viumbe sita vyenye hali tofauti na uwafunge pamoja kwa kamba ngumu na uwaachie waondoke. Kila mmoja wao atajaribu kurudi katika makao yake kwa njia yake: nyoka atatafuta nyasi ndefu, mamba atatafuta maji, ndege atahitaji kuruka angani, mbwa atatafuta kijiji, mbweha atatafuta nyika na nyani atatafuta miti ya msituni. Katika jitihada ya kutaka kujinasua kila mmoja aende vyake kutakuwa na mapambano, lakini kwa kuwa wote wamefungwa katika kamba moja, mwenye nguvu zaidi ya wote atawavuta wote.

Kama viumbe katika mfano huu, binadamu hujaribiwa kwa njia nyingi kwa tamaa za milango yake ya fahamu sita, macho, masikio, pua, ulimi, mguso na moyo, na vyote vinatawaliwa na tamaa.

Ikiwa viumbe hao sita watafungwa kwenye mlingoti, watajitahidi kujinasua hadi hapo kila mmoja atakapochoka na kulala chini ya mlingoti. Vivi hivi, ikiwa watu watajifunza na kuutawala moyo hapatakuwepo na milango mingine mitano ya fahamu. Ikiwa moyo utatawaliwa watu watakuwa na furaha tangu sasa hata siku zijazo.

4. Watu hupenda faraja ya binafsi ambayo ni mapenzi ya umaarufu na sifa. Lakini sifa na umaarufu ni sawasawa na ubani uunguao kwa nguvu na hatimaye kuisha. Ikiwa watu watatafuta utukufu na heshima kutoka kwa watu na kuacha njia ya ukweli, wako katika hatari kubwa na hatima yake watakuwa na sababu ya kujuta.

Mtu ambaye hutafuta sifa na utajiri na mambo ya mapenzi ni sawa na mtoto ambaye hulamba asali kutoka kwenye makali ya kisu. Anapoonja utamu wa asali kuna hatari ya kuumiza ulimi wake. Mtoto huyo anafananishwa na mtu abebaye mwenge akiukabili upepo; bila shaka miale ya moto itamuunguza uso na mikono yake.

Mtu asiamini moyo wake uliojaa uchoyo hasira na ujinga. Mtu asiruhusu moyo wake ukimbie ovyo bali autawale kabisa.

5. Kuupata uwezo wa kuutawala moyo ni jambo gumu sana. Wale wautafutao Wongofu yawapasa kwanza waondokane na moto wa tamaa zote. Tamaa ni moto uwakao kwa kishindo hivyo mtu atafutaye Wongofu yampasa kukwepa moto wa tamaa kama

mtu aliyebeba mzigo wa nyasi kavu anavyokwepa cheche za moto.

Lakini itakuawa ujinga mtupu kwa mtu kufumba macho eti kwa sababu ya kuogopa kujaribiwa kutokana na sura nzuri atakazoziona. Moyo ndio kiongozi kwa hiyo kama unaweza kutawaliwa tamaa ndogo zitakwisha.

Ni vigumu kutafuta njia ya Wongofu, lakini ni vigumu zaidi ikiwa watu hawana moyo wa kuitafuta njia kama hiyo. Bila ya Wongofu kuna mateso yasiyokoma katika dunia ya kufa na kupona.

Mtu anapotafuta njia ya Wongofu inakuwa kama ng'ombe abebaye mzigo mzito huku akipita katika tope zito. Ikiwa maksai huyo atajitahidi kwa nguvu zake zote bila kushughulikia mambo mengine anaweza akayavuka matope salama na akapumzika. Kwa hiyo, moyo ukitawaliwa barabara na kuelekezwa katika njia sahihi, hapatakuwepo na tope la uchoyo la kuuzuia na mateso yake yote yatakwisha.

6. Wote wafuatao njia ya Wongofu yawapasa kuondokana na aina zote za majivuno ya ubinafsi na wawe tayari kwa unyenyekevu kupokea mwanga wa mafundisho ya Buddha. Hazina zote za dunia, dhahabu yake yote na fedha yake yote na heshima, haviwezi kulinganishwa na hekima na uadilifu.

Ili kufurahia afya bora, kupata furaha ya kweli kwa familia

ya mtu, kuleta amani kwa wote, ni lazima mtu awe na nidhamu na atawale moyo wake. Mtu akiweza kuutawala moyo wake anaweza kuipata njia ya wongofu, na hivyo hekima na wema wote vitakuja kwake.

Kama hazina inavyochimbuliwa kutoka ardhini vivyo hivyo wema hutokana na matendo mema, na hekima hutokana na moyo safi wenye amani. Ili kutembea kwa usalama katika mashaka ya maisha ya binadamu, mtu anahitaji mwanga wa hekima na mwongozo wa uadilifu.

Mafundisho ya Buddha, ambayo yanaeleza watu jinsi ya kuondokana na uchoyo, hasira na ujinga ni mafundisho mema na watu wote wanaoyafuata hupata maisha mazuri na ya furaha.

7. Binadamu wanatabia ya kufuata uelekeo wa mawazo yao. Wanapokuwa na fikra za uchoyo nao huwa wachoyo; Wakiwa wana fikara za hasira, wanakuwa na hasira zaidi; Wakishiriki fikra za kijinga, wataelekea katika ujinga.

Wakati wa mavuno wakulima hufungia mifugo yao isije ikavunja ugo na kuingia katika mashamba ya watu ikasababisha malalamiko mengi au kuuawa; hivyo basi watu yawapasa kuchunga mioyo yao kutokana na udanganyifu na taabu. Lazima waondokane na fikra zinazochochea uchoyo, hasira na ujinga, Ila washawishi fikra zinazochochea huruma na fadhila.

Wakati wa mvua za vuli malisho hujaa nyasi na wafugaji

wakati huo hufungulia mifugo yao lakini hata hivyo mifugo hawaachwi bila mchungaji. Ndivyo ilivyo hata kwa mioyo ya watu: Hata wakati wa hali nzuri moyo lazima ulindwe.

8. Wakati fulani Shakyamuni Buddha aliishi katika mji wa Kausambi. Katika mji huo alikuwepo Bwana mmoja aliyemchukia Buddha hadi akachukua hatua za kuwahonga watu wabaya waeleze hadithi za owongo juu yake. Katika hali kama hiyo ilikuwa vigumu sana kwa wanafunzi wake kupewa chakula cha kutosha kila waombapo pia matusi mengi katika mji huo yaliwaandama.

Ananda alimwambia Shakyamuni; "Ni heri tuondoke katika mji huo. Kuna miji mingine bora tunakoweza kwenda. Afadhali tuondoke hapa."

Aliyebarikiwa alijibu: "Je ikiwa mji mwingine utakuwa kama huu tutafanyaje?"

"Basi tutakwenda katika mji mwingine"

Aliyebarikiwa alisema: Hapana, Ananda, katika hali hiyo hatutatulia. Afadhali tuendelee kukaa hapa tukayavumilie matusi hadi yatakapoisha ndipo twende katika mji mwingine.

Kuna faida na hasara, visingizio na heshima, sifa na matusi, mateso na furaha katika dunia hii. Mwongofu hatawaliwi na

mambo haya ya nje; yatatoweka kwa haraka sana kama yanavyokuja.

## II
## NJIA BORA YA KUTENDA MEMA

1. Wale waitafutayo njia ya Wongofu ni lazima wakumbuke umuhimu wa kuiweka safi miili yao, maneno na mioyo yao. Kuiweka miili yao nadhifu yampasa mtu asiue kiumbe chochote, asiibe, au kuwa mzinzi. Ili kuwa na lugha safi mtu yampasa asidanganye au kutukana au kuongopa au kujihusisha katika mazungumzo yasiyo na maana. Ili kuwa na moyo safi yampasa mtu aondokane na aina zota za uchoyo, hasira na maamuzi potofu.

Ikiwa moyo utakuwa mchafu, hakika hata matendo ya mtu yatakuwa machafu; ikiwa matendo yatakuwa machafu kutakuwepo na mateso. Kwa hiyo ni jambo la muhimu sana mwili, mdomo na moyo vikawekwa safi.

2. Zama zile kulikuwa na mjane aliyekuwa tajiri mwenye sifa ya huruma, adabu na ukarimu. Alikuwa na mfanyakazi mwenye hekima na juhudi.

Siku moja mfanyakazi wake alifikiri : "Mkuu wangu ana sifa nzuri sana; sijui kama ni nzuri kwa asili yake au ni nzuri kwa sababu ya mazingira yake. Nitamjaribu ili nijue ukweli."

Asubuhi iliyofuata mfanyakazi huyo hakuonekana machoni pa mkuu wake hadi adhuhuri. Mkuu wake alipatwa na ghadhabu akamsuta vikali bila huruma. Mfanyakazi alijibu:
"Ikiwa mimi ni mvivu siku moja au siku mbili, hupaswi kukosa subira". Hapo mkuu wake alipandwa na hasira.

Siku iliyofuata mfanyakazi huyo alichelewa tena kuamka mapema. Kitendo hicho kilimfanya mjane akasirike sana hata akaamua kumchapa kwa fimbo. Habari za tukio hilo zilienea kila sehemu, na majane huyo tajiri akawa amepoteza sifa yake njema.

3. Watu wengi wako kama mama huyo. Mazingira yao yanapojitosheleza wanakuwa na huruma, adabu njema na wakimya, lakini haielezeki ikiwa wanaweza kuendelea na tabia hiyo wakati hali ya mambo inapobadilika na ikawa hairidhishi.

Ni pale tu mtu anapoendelea kudumisha moyo safi na wenye amani na kutenda wema wakati maneno mabaya yanapoingia masikioni mwake, watu wengine wanapomchukia au anapokosa chakula cha kutosha, mavazi na nyumba , hapo huenda tukamwita mwema.

Kwa hiyo basi, wale watendao matendo mema na kudumisha moyo wa amani tu wakati mazingira yao yanajitosheleza hao hakika siyo watu wema. Ni wale tu waliyoyapokea mafundisho ya Buddha na wakayafunza kwa mioyo na miili yao mafundisho hayo hao wanaweza kuitwa watu wema na wenye adabu njema na amani.

4. Kuhusu ubora wa maneno ya kutumia, kuna jozi tano za kinyume: Maneno ambayo ni bora katika nafasi zake na yale yasiyo bora kwa nafasi hizo; maneno ambayo yanafaa kwenye ukweli na yale yasiyofaa; maneno yenye utamu na yale ya kejeli; maneno yenye faida na yale yenye hasara; na maneno yenye huruma na yale yenye chuki.

Maneno yoyote yale tunayozungumza ni bora tuyachague kwa makini kwa sababu watu watayasikia na huenda yakawashawishi kwa wema au ubaya. Ikiwa mioyo yetu itajaa huruma na utu wema, itahimili maneno maovu tuyasikiayo. Tusikubali kamwe maneno machafu kutoka midomoni mwetu yasije yakaamsha hisia ya chuki na hasira. Maneno tunayoyazungumza daima yawe ni ya upole na hekima daima.

Fikiria mtu anayekusudia kuzoa takataka kutoka kwenye uwanja. Akatumia beleshi na ungo na akafanya kazi kwa bidii akitawanya takataka huko na huko, lakini ni kazi ngumu. Kama mjinga huyo hatuwezi kutumainia kutupilia mbali maneno yote. Lazima tuizoeze akili yetu na tujaze mioyo yetu kwa upole na wema ili tusisumbuliwe na maneno yasemwayo na watu wengine.

Mtu anaweza akajaribu kuchora picha kwa maji ya rangi kwenye anga ya bluu, lakini hii haiwezekani. Vilevile haiwezekani kukausha mto mkubwa kwa joto la tochi iliyotengenezwa kwa nyasi kavu za kulishia ng'ombe, au kutoa sauti isababishayo mipasuko kwa kusugua vipande viwili vya

ngozi laini. Watu lazima wazoeze akili zao kama mifano hiyo miwili ili wasivurugwe na maneno yoyote wanayoweza kuyasikia.

Yawapasa kufunza akili na mioyo yao na kuipanua kwa mapana ya dunia, isiwe na mipaka kama mbingu, yenye kina kirefu kama mto mkubwa, na laini kama ngozi iliyotiwa dawa ya kuilainisha.

Hata kama adui yako akikukamata na kukutesa, ukipandwa na hasira hutakuwa unafuata mafundisho ya Buddha. Katika hali yoyote ile huna budi kujifunza kufikiri: "Moyo wangu hauteteleki. Maneno ya chuki na hasira hayawezi kutoka mdomoni mwangu. Nitamzungushia adui yangu mawazo yenye wema, upole,yanayotokana na moyo uliojaa huruma katika hali zote za maisha."

5. Kuna hadithi inayozungumzia juu ya bwana mmoja aliyepata kukiona kichuguu kilichokuwa kinaungua mchana, na usiku kinafuka moshi. Alikwenda kwa mtu mwenye busara na akamwomba ampe ushauri kuhusu jambo ambalo anaweza kutenda. Yule mtu mwenye busara akamwambia kuchimba katika kichuguu kwa kutumia sime. Yule bwana alifanya hivyo. Naye alipata kwa mpangilio vitu vifuatavyo:- Ufito wa chuma, mapovu ya maji, pande la chuma, sanduku, kobe, kisu kikali, kipande cha nyama na mwisho likatoka joka. Bwana huyo alikwenda kutoa taarifa kuhusu aliyoyaona. Mwenye busara alifafanua umuhimu wa mambo hayo na akasema, "tupilia mbali

kila kitu isipokuwa joka; liache hilo joka na wala usilisumbue."

Hii ni ngano ambayo kwayo "kichuguu" ina maana ya mwili wa binadamu. "Kilichokuwa kinaungua "mchana kutwa" ina maana kwamba wakati wa mchana watu hutenda matendo waliyoyafikiria usiku uliotangulia. "Kinafuka moshi usiku" inaelezea ukweli kwamba watu wakati wa usiku hukumbuka kwa furaha au hujuta kutokana na mambo waliyoyafanya wakati wa mchana.

Katika ngano hiyo hiyo, "Bwana " ina maana mtu atafutaye Wongofu. "Mtu mwenye busara" maana yake ni Buddha. "Sime" ina maana ya hekima. "Chimba katika kichuguu" inaeleza juu ya juhudi zinazohitajika ili kuupata Uongofu.

Tena katika ngano hiyo hiyo, "ufito wa chuma wa lango" ina maana ya ujinga; "Mapovu" ni vishindo vya sauti za mateso na hasira; "pande la chuma" inaashiria kusita na kutokuwa tayari, "Sanduku" ina maana uwekaji wa hasira, uchoyo, uvivu, ugeugeu, majuto na madanganyo; "kobe" ina maana ya mwili na roho; kisu kikali ina maana ya mchanganyiko wa tamaa tano za fahamu, na "kipande cha nyama" ina maana ya matokeo ya tamaa imfanyayo mtu kutamani baada ya kutosheka. Vitu vyote hivyo ni hatari kwa binadamu, kwa hiyo Buddha alisema, "Tupilia mbali kila kitu.

Zaidi ya hapo, "joka" inaashiria moyo ambao umetupilia mbali mateso ya duniani ikiwa mtu atachimba katika mambo yake

kwa singe ya hekima hatimaye atalifikia joka lake. "Liache joka hilo na wala usilisumbue" ina maana ya kufuatilia na kuuchimba moyo ambao uko huru na tamaa za kidunia.

6. Pindola, mwanafunzi wa Buddha baada ya kupata Wongofu alirudi kwao Kausambi kutoa shukrani kwa watu wa huko kutokana na wema waliomtendea. Katika kufanya hivyo alikuwa ameandaa shamba kwa ajili ya kupanda mbegu za ki-Buddha.

Katika viungo vya Kausambi kuna mbuga ndogo kandokando ya mto Ganges iliyofunikwa na sufu ndefu za minazi ikipulizwa na upepo mwanana.

Siku moja, wakati wa kiangazi, Pindola alikaa ili atafakari chini ya kivuli cha mti wakati mfalme Udayana alipofika katika mbuga hiyo akiwa ameambatana na wenzi wake ili wakastarehe huko, na baada ya starehe na muziki mfalme alijipumzisha chini ya kivuli cha mti mwingine.

Wakati Mfalme wao akiwa amelala usingizi, wake zake na mabibi waliomsubiri walitembeatembea na ghafla wakamkuta Pindola amekaa katika kutafakari. Walimtambua kama mtu mtakatifu, wakamuomba awafundishe nao wakasikiliza maubiri yake.

Mfalme alipozinduka usingizini aliondoka kuwatafuta bibi zake na akawakuta wamemzunguka huyo mwanamme na huku

wakisikiliza mafundisho yake. Akiwa na moyo wa wivu na tamaa ya wanawake, Mfalme alijawa hasira na akamtukana Pindola akisema; "Ni jambo lisilosameheka kwako, mtu mtakatifu kuwa katikati ya wanawake huku ukifurahia mazungumzo ya kipuuzi pamoja nao." Pindola alifumba macho yake kwa haraka na akakaa kimya.

Akiwa amejaa hasira, Mfalme alichomoa sime na kumtisha Pindola, lakini mtu huyo wa Mungu alikaa kimya na imara kama mwamba. Hii ilimfanya Mfalme akasirike zaidi kwa hiyo akapasua kichuguu na kumtupia takataka zote zilizotoka humo lakini bado Pindola aliendelea kukaa kimya akaendelea kukaa katika kutafakari, akivumilia matusi na maumivu.

Baadaye, Mfalme alishikwa na aibu kutokana na tabia yake ya kikatili hivyo akamwomba Pindola msamaha. Kutokana na tukio hili mafundisho ya Buddha yalipata njia ya kuingia katika ngome ya Mfalme na kutoka humo yalisambaa katika nchi nzima.

7. Siku chache baadaye Mfalme Udayana alimtembelea Pindola katika sehemu yake ya maombi msituni alipoishi na akamuuliza, "Mwalimu mwenye kuheshimika, inawezekanaje wanafunzi wa Buddha kutunza miili yao safi na mioyo yao safi bila ya majaribu ya uzinifu ingawa wengi wao bado vijana?"

Pindola alijibu: "Bwana Mheshimiwa, Buddha ametufundisha kuheshimu wanawake wa makamo kama mama zetu, kuwaheshimu wake wa rika letu kama dada zetu na wale

wadogo tuwaheshimu kama binti zetu. Kutokana na mafundisho haya wanafunzi wa Buddha wanauwezo wa kutunza miili yao safi na bila majaribu ya uzinifu ingawa ni vijana."

"Lakini mwalimu mheshimiwa mtu anaweza kuwa na mawazo machafu juu ya mwanamke mwenye umri wa mama yake au dada yake au binti yake. Je wanafunzi wa Buddha wanatawalaje tamaa zao?"

"Bwana mheshimiwa, Aliyebalikiwa alitufundisha kuiona miili yetu kama itoayo uchafu wa aina zote kama vile damu, usaa, jasho na mafuta; kwa kuwazia hivyo, sisi, ingawa tu vijana, tunaweza kutunza mioyo yetu kwa usafi."

"Mwalimu mheshimika," Mfalme aliendelea kusisitiza. "Hii inawezekana kwa kuwa umezoeza mwili na moyo wako na kusafisha hekima yako , bali itakuwa vigumu kwa wale ambao bado hawajapata mafundisho ya namna hiyo. Wanaweza kujaribu kukumbuka uchafu lakini macho yao yatafuatilia sura nzuri. Wanaweza kujaribu kuona ubaya wa sura, lakini watavutiwa kwa hali ile ile na sura nzuri sana. Lazima kuna sababu nyingine inayowafanya vijana kati ya wanafunzi wa Buddha kuwa na matendo safi."

"Bwana mheshimiwa," alijibu Pindola, "Aliyebarikiwa hutufundisha kuchunga milango mitano ya fahamu. Tunapoangalia maumbo mazuri na rangi kwa macho yetu, tunaposikia sauti nzuri kwa masikio yetu, tunaponusa harufu

nzuri kwa pua yetu, au tunapoonja vitu vitamu kwa ulimi wetu au kugusa vitu vyelolo kwa mikono yetu hatupaswi kutawaliwa na vitu hivi vinavyotamanisha wala hatuwezi kukomeshwa na vitu visivyo vutia. Tunafundishwa kulinda milango mitano ya fahamu kwa makini. Ni kutokana na mafundisho ya Aliyebarikiwa, ambayo kwayo hata wanafunzi vijana wanaweza kutunza miili na mioyo yao kwa usafi."

"Mafundisho ya Buddha ni ya ajabu kweli kweli. Kutokana na uzoefu wangu binafsi nafahamu kuwa nikumbanapo na kitu chochote kizuri, bila kujilinda nasumbuliwa na vishawishi vya milango ya fahamu. Ni jambo la msingi kulinda milango mitano ya fahamu wakati wowote ili kuwa na matendo safi."

8. Mtu anapokueleza mawazo ya moyo wake katika matendo hali ya malipizo hufuata. Mtu akikutupia matusi, kuna majaribu ya kujibu au kulipiza kisasi. Ni lazima mtu ajilinde kutokana na hali ya kawaida ya kutaka kulipiza mambo. Ni sawasawa na kutema mate katika upepo, hayampati mtu yeyote isipokuwa yule aliyeyatema, ni sawasawa na kufagia vumbi katika upepo, kujichafua mwenyewe. Misiba hufuata hatua za mtu anayetoa nafasi au njia ya tamaa ya kulipiza kisasi.

9. Ni tendo zuri sana kuachana na uchoyo na kuhifadhi upendano. Bado ni bora kulinda nia ya moyo juu ya kuheshimu Njia Bora.

Yampasa mtu kuondokana na moyo wa ubinafsi na kuwa

na moyo wenye unyenyekevu wa kuwasaidia wengine. Tendo la kumfanya mtu mmoja awe na furaha humtia moyo mtu mwingine kumpa furaha mwenzake, hivyo furaha huwepo kutokana na tendo la namna hiyo.

Maelfu ya mishumaa inaweza kuwashwa kutokana na mshumaa mmoja, na maisha ya mshumaa yatakuwa mafupi. Furaha haipungui kutokana na tendo la kuigawana.

Watu wanaoutafuta Uongofu lazima wawe makini kwa kila hatua wanayoichukuwa. Hata kama matakwa ya mtu yatakuwa makubwa sana lazima yapatikane hatua kwa hatua. Hatua za njia ya Wongofu lazima zichukuliwe katika hatua yetu ya kila siku.

10. Mwanzoni mwa njia ya Wongofu kuna mambo magumu katika dunia hii ambayo lazima tuyashinde, nayo ni:- 1. Ni vigumu kwa mtu maskini kuwa mkarimu. 2. Ni vigumu kwa mtu mwenye majivuno kujifunza Njia ya Uongofu. 3. Ni vigumu kuutafuta Uongofu kwa gharama ya kujitoa kafara. 4. Ni vigumu kuzaliwa wakati Buddha yuko duniani. 5. Ni vigumu kusikia mafundisho ya Buddha. 6. Ni vigumu kuwa na moyo safi kushindana na silika za mwili. 7. Ni vigumu kutotamani vitu vizuri na vinavyovutia. 8. Ni vigumu kwa mtu mwenye nguvu kushindwa kutumia nguvu zake kutosheleza tamaa zake. 9. Ni vigumu mtu kutopandwa na hasira wakati ameudhiwa. 10. Ni vigumu kukaa bila hatia mtu anapojaribiwa na mambo ya ghafla. 11. Ni vigumu mtu binafsi kuomba kujifunza kwa mapana na makini. 12. Ni vigumu kutomdharau mtu anayeanza. 13. Ni

vigumu mtu kuwa mnyenyekevu. 14. Ni vigumu kupata marafiki wema. 15. Ni vigumu kuvumilia nidhamu inayoelekeza kwenye Uongofu. 16. Ni vigumu kutokusumbuliwa na mambo ya nje. 17 Ni vigumu kuwafundisha wengine kwa kufahamu uwezo wao. 18. Ni vigumu kuwa na moyo wa amani. 19. Ni vigumu kutokubishana juu ya wema na ubaya. 20. Ni vigumu kubuni na kujifunza njia mpya.

11. Watu wema na wabaya hutofautiana katika hali zao. Watu wabaya hawayatambui matendo mabaya kama ni ya dhambi; ubaya wa matendo hayo unapoelezwa kwao, hawayaachi kuyatenda na hawataki mtu aendelee kuwaonya juu ya matendo yao mabaya. Watu wema huguswa sana na mema na mabaya; huacha kutenda jambo lolote lile walionalo kuwa ni baya; humshukuru mtu yeyote yule anayewaonya juu ya matendo mabaya hayo.

Kwa hiyo watu wema na wabaya hutofautiana vibaya sana. Watu wabaya hawatambui wema wanaotendewa, lakini watu wenye busara hutambua na kushukuru. Watu wema hujaribu kuwaeleza utambuzi wao, furaha na shukrani kwa kulipa wema, sio kwa wafadhili bali kwa mtu yeyote.

# III
# MAFUNDISHO KATIKA HADITHI ZA KALE

1. Hapo kale kulikuwa na nchi iliyokuwa na desturi ya pekee ya kuwatupa wazee porini na milimani kusikofikika.

Waziri mmoja wa Serikali aliona vigumu kufuata desturi hii kuhusu baba yake. Hivyo kwa siri alijenga pango chini ya ardhi akamtunza baba yake humo.

Siku moja muungu alimtokea Mfalme wa nchi hiyo na akampa fumbo la kutatanisha akisema kuwa akishindwa kufumbua fumbo hilo kwa ukamilifu, nchi yake itaaribiwa: Fumbo lilikuwa : "Kuna nyoka wawili hapa; nitajie jinsia ya kila mmoja."

Hakuna mtu hata mmoja aliyeweza kufumbua fumbo hilo; hivyo Mfalme alitoa zawadi kubwa kwa mtu yoyote katika miliki yake atakayefumbua fumbo hilo.

Yule waziri alikwenda kwenye maficho ya baba yake na kumuuliza jibu la fumbo hilo. Mzee alisema:- "Ni jibu rahisi sana. Waweke nyoka wawili kwenye zuria laini; yule atakayejongea ndiye dume, na yule atakayetulia ni jike." Waziri alimpelekea Mfalme jibu hilo na fumbo likawa limefumbuliwa.

Pia muungu aliuliza maswali mengine magumu

yaliyomshinda Mfalme pamoja na wafuasi wake, lakini baada ya waziri kushaurina na baba yake mzee aliweza kuyajibu.

Yafuatayo ni baadhi ya maswali na majibu yake "Ni nani huyo, anapokuwa amelala usingizi, huitwa aliye macho, na, anapokuwa macho, huitwa aliyelala?" jibu lake ni:- Ni yule anayepata mafundisho ya Uongofu. Yu macho anapolinganishwa na wale waliokwisha kupokea Uongofu.

"Unawezaje kupima uzito wa tembo mkubwa?"

"Mweke tembo katika mashua na weka alama kwenye mashua kuonyesha mzamo wake kisha ujaze mawe katika mashua hadi izamapo kufikia alama uliyoichora. Pima uzito wa mawe."

Nini maana ya methali, "kikombe cha maji ni bora kuliko maji ya bahari?" Hili ndilo jibu lake . "Kikombe cha maji kilichotolewa kwa roho njema na ya huruma kwa wazazi wa mtu au mgonjwa kina sifa ya milele, lakini maji ya bahari kuna siku moja yatakauka."

Tena muungu alitengeneza mtu anayekufa njaa, amebakia mifupa na ngozi tu, akilalamika, "Kuna mtu yeyote duniani mwenye njaa, kuliko mimi?" "Mtu mwenye ubinafsi na uchoyo kiasi kwamba haamini katika hazina Tatu za Buddha, Dharma, na Samgha, na ambaye hatambikii wazazi na walimu wake, sio kwamba ana njaa sana bali ataanguka katika dunia ya mapepo ya njaa na huko atapata mateso ya njaa milele."

"Hapa kuna ubao wa mti wa Chandana, ni sehemu gani ya ubao huo ambayo inaelekea kwenye kitako cha shina la mti?" "Weka ubao ndani ya maji; Sehemu ya ubao itakayo zama zaidi ndani ya maji itakuwa sehemu ya mwisho iliyokuwa karibu na shina la mti."

"Hapa kuna farasi wawili wanaolingana na kufanana. Utawezaje kutambua ni yupi mtoto na yupi ni mama?." "Wape majani kidogo, mama atasukuma majani hayo kwa mtoto."

Kila jibu la maswali haya magumu liliwafurahisha muungu na Mfalme pia. Mfalme alishukuru sana alipogundua kuwa majibu haya mazuri yalitoka kwa mzee baba yake waziri aliyekuwa amemficha pangoni na akafuta sheria ya kuwatupa wazee milimani na akaamuru watunzwe kwa upole na ukarimu.

2. Siku moja Malkia wa Videha wa India alimuota tembo mweupe mwenye meno sita. Alitamani pembe hizo na akamuomba mfalme amtafutie pembe hizo ingawa kazi ya kupata pembe hizo ilikuwa ngumu, Mfalme aliyempenda sana Malkia alitoa taarifa ya kumuona tembo wa namna hiyo.

Ilitokea kwamba kulikuwa na tembo wa namna hiyo katika Milima ya Himalaya aliyekuwa anajifunza u-Buddha. Wakati fulani tembo huyu aliokoa maisha ya mwindaji katika hali ya hatari katikati ya milima. Mwindaji huyo alipata bahati ya kurudi katika nchi yake salama salimini. Hata hivyo, akiwa amepofushwa

na ukubwa wa zawadi na usahaulifu wa wema aliotendewa na tembo huyo, mwindaji alirudi milimani ili amuue.

Mwindaji, akiwa anajua kwamba tembo alikuwa anatafuta u-Buddha, alijifunika katika vazi la utawa wa ki-Buddha, akamkaribia tembo bila matata, akamchoma kwa mshale wa sumu.

Tembo akitambua kwamba mwisho wake umekaribia na kwamba mwindaji alikuwa ametekwa na tamaa ya kidunia kwa ajili ya zawadi, alipatwa huruma juu yake, akamfunika katikati ya ghadhabu kali ya tembo wengine waliotaka kulipiza kisasi. Hapo tembo alimuuliza mwindaji kwanini alikuwa amemtendea tendo la kijinga kama hilo. Mwindaji alimwambia juu ya zawadi na akatubu kwamba alitamani meno sita. Mara moja tembo aliyakata meno yake kwa kuyagonga kwenye mti na kumkabidhi mwindaji akisema:- "Kwa sadaka hii nakamilisha mafundisho yangu ya u-Buddha na nitazaliwa tena katika nchi takatifu. Nitakapokuwa Buddha nitakusaidia kuondoa mishale mitatu ya sumu ya uchoyo, hasira na ujinga."

3. Katika msitu chini ya Milima Himalaya palikuwepo na kasuku aliyeishi pamoja na wanyama na ndege wengine wengi. Siku moja moto ulizuka katika msitu huo kutokana na msuguano wa mianzi kukiwa na upepo mkali na hivyo wanyama na ndege waliingiwa na hali ya hofu. Kasuku akiwa na huruma kwa hofu na mateso yao, na akiwa anataka kulipa wema aliokuwa akipata katika msitu wa mianzi uliokuwa ukimpatia hifadhi, alifanya kila

lililowezekana ili awaokoe. Akajizamisha katika bwawa lililokuwa karibu na akaruka juu huku akijitikisa na kudondosha matone ya maji juu ya moto akiwania kuuzima. Aliendelea kufanya hivyo kwa bidii, na kwa moyo wa huruma, na kutoa shukrani kwenye msitu.

Roho ya wema na ya kujitoa mhanga ilitambuliwa na muungu huko mbinguni aliyetelemka kutoka angani na kumwambia kasuku:-"Una moyo hodari, lakini unatarajia mafanikio yapi kutokana na matone machache uyadondoshayo juu ya moto mkubwa?" Kasuku alijibu:- "Hakuna jambo lisilowezekana kutokana na moyo wa shukrani na kujitoa mhanga. Nitajaribu tena na tena, zaidi na zaidi katika maisha yajayo." Muungu mkuu alifurahishwa na roho ya kasuku na kwa pamoja wakauzima moto.

4. Wakati fulani ndege mwenye vichwa viwili kwenye mwili mmoja aliishi katika milima ya Himalaya. Siku moja kichwa kimoja kilikiona chenzake kikila matunda matamu na kikaona wivu na kujisemea:- "Basi mimi nitakula tunda lenye sumu." Kwa hiyo kikala sumu na ndege mzima akafa.

5. Wakati mwingine pia kichwa na mkia wa nyoka viligombania kutangulia. Mkia alimwambia kichwa:- "Kila siku unatangulia; Sio usawa niachie nami nitangulie nyakati fulani." Kichwa alijibu:- "Ni sheria ya maumbile mimi kuwa kichwa; hatuwezi kubadilishana."

Katika maumbile ya dunia kuna utaratibu sahihi na kila kitu kina kazi yake maalum. Kanuni hii inapovurugwa, utendaji kazi unaingiliwa, na utaratibu mzima unaharibika.

6. Kulikuwa na mwanamme aliyekuwa anaghadhabika kwa urahisi. Siku moja watu wawili walikuwa wanazungumza mbele ya nyumba juu ya bwana aliyeishi humo. Mmoja alimwambia mwenzake:- "Ni mtu mwema lakini hana simile; ana gadhabu kali na hukasirika mara moja." Huyo bwana aliyasikia yale maneno, bila kukusudia, alichomoka ndani ya nyumba na kuwashambulia wale watu wawili kwa kuwachapa, kuwapiga mateke na kuwajeruhi.

Mtu mwenye busara anaposhauriwa juu ya makosa yake, atajirudi na kubadilisha mwenendo wake. Mtu mjinga anaposhauriwa juu ya tabia yake mbaya hatadharau tu ushauri bali atarudia kosa lilelile.

7. Hapo kale palikuwa na tajiri mmoja mjinga. Alipoiona nyumba nzuri ya bwana mmoja yenye ghorofa tatu akaona wivu na akakata shauri kujenga nyumba kama hiyo akifikiri kuwa mwenye nyumba naye ni tajiri. Alimwagiza fundi aijenge. Bwana fundi alikubaliana naye na mara moja akaanza kujenga msingi, ghorofa ya kwanza, ghorofa ya pili, na mwisho ghorofa ya tatu. Tajiri huyu aliangalia kazi yake kwa machukizo na kusema:- "Sihitaji msingi, ghorofa ya kwanza, au ghorofa ya pili; nataka ghorofa nzuri ya tatu. "Ijenge haraka"!

8. Siku moja mpumbavu alikuwa akichemsha asali. Ghafla alitokea rafiki yake na kwa kuwa huyo mpumbavu alitaka ampe asali, lakini kwa vile ilikuwa bado ikichemka aliamua kuipembea ili ipoe bila kuitoa motoni. Vivyo hivyo ni vigumu kupata asali ya hekima iliyotulia bila kuitoa kutoka katika moto wa mateso ya dunia.

9. Siku moja kulikuwa na mapepo wabaya wawili walioshinda kutwa wakibishana na kuzozana juu ya sanduku, henzerani na jozi ya viatu. Mpita njia mmoja aliuliza, "kwa nini mnabishana kuhusu mambo haya? Vitu hivyo vina nguvu gani za miujiza zinazowafanya muendelee kubishana na kuzozana kuhusu umilikaji wake." Mapepo yalimweleza kuwa kutoka katika sanduku yangeweza kupata chochote walichokihitaji-Chakula, mavazi au hazina, kwa kutumia henzerani yangeweza kuwashinda adui zao wote; na kwa kutumia jozi ya viatu wangeweza kusafiri kupitia angani.

Baada ya kuyasikia haya, yule mpita njia alisema:-"Kwa nini kuzozana? Kama mnaweza kutoweka hapa kwa dakika chache, naweza kufikiria mgawano ulio bora kwa vitu hivyo kati yenu." Kwa hiyo mapepo mawili yaliondoka na mara tu baada ya kuondoka mpita njia alivaa vile viatu, akachukua sanduku na henzerani na akatawanyika kupitia hewani.

"Mapepo" yanawakilisha watu wasiokuwa na dini. "Sanduku" ina maana ya zawadi zitolewazo kwa hisani; hawaelewi ni kiasi gani cha hazina kinachoweza kupatikana

kutokana na uhisani "Henzerani" ina maana ya mazoea ya kutuliza fikara kwa makini. Watu hawaelewi kuwa maisha ya roho ya kutuliza fikara kwa moyo wanaweza kushinda tamaa za kidunia. "jozi ya vitu ina maana nidhamu safi ya mawazo na matendo itakayo wavusha katika ng'ambo ya tamaa zote na mabishano. Bila ya kutambua hayo hubishana na kuzozana juu ya sanduku, henzirani na jozi ya viatu.

10. Zamani za kale bwana mmoja alikuwa anasafiri peke yake. Ilipokaribia jioni alifikia kwenye nyumba isiyokuwa na mtu akaamua kulala humo. Yapata usiku wa manane jini lilileta maiti ndani ya nyumba hiyo na kuiacha kwenye sakafu. Kitambo kidogo jini jingine lilitokea kudai kwamba maiti ilikuwa yake likaanzisha mzozo.

Kisha jini la kwanza lilisema kuwa ni kazi bure kuendelea kubishana na likashauri kesi hiyo ipelekwe kwa hakimu atakayeamua ni nani mwenye haki. Jini jingine lilikubaliana na wazo hilo ila kwa kumuona mtu aliyejibanza pembeni kwa woga yakamkamata atoe uamuzi. Mwanamme huyo alipatwa na hofu kwa kujua kuwa uamuzi atakao toa utalikasirisha jini mojawapo na hilo litakalokasirika huenda likaamua kulipiza kisasi. Hata hivyo aliamua kueleza ukweli alioushuhudia.

Kama alivyotarajia, uamuzi wake ulimuudhi jini wa pili na hivyo jini lilimshika mkono wake mmoja kwa nguvu likaurarua lakini jini la kwanza liliurudishia kwa kutumia mkono mwingine wa maiti aliyekuwa sakafuni. Jini la pili kwa hasira liliurarua

mkono wake wa pili lakini jini la kwanza likarudishia mkono mwingine wa maiti mara moja. Mambo yaliendelea vivyo hivyo hadi mikono yote, miguu yote, kichwa na kiwiliwili vikawa vimeraruliwa na kuwekewa sehemu kama zile za mwili wa maiti. Majini yalipoona vipande vya mwili wa yule bwana vimesambaa sakafuni yaliviokota yakavila vyote na kuondoka kwa kicheko cha kichini chini.

Maskini aliyekuwa amejificha katika nyumba alikaraishwa na mikasa iliyomsibu. Sehemu za mwili wake zilizoliwa na majini alizirithi kwa wazazi wake na sehemu alizokuwa nazo zilikuwa za maiti. Hivi yeye alikuwa nani? Kwa kutotambua yeye ni nani na kwa kuchanganyikiwa alitoka ndani ya nyumba hiyo na kutembeatembea nje. Alipoliona hekalu, aliingia ndani na akawaelezea watawa matatizo yake. Watu waliuona ukweli na maana ya kutokuwa na ubinafsi kutokana na masimlizi yake.

11. Siku moja mrembo mmoja aliyevalia maridadi alitembelea nyumba moja. Mwenye nyumba alimuuliza yeye ni nani naye akajibu kuwa yeye ni muungu wa utajiri. Mwenye nyumba alifurahi na akampatia mapokezi mazuri.

Kitambo kidogo, alitokea mwanamke mwenye sura mbaya na mavazi machakavu. Mwenye nyumba alimuuliza yeye ni nani naye akamueleza kuwa alikuwa muungu wa umaskini. Mwenye nyumba aliogopa sana na akajaribu kumfukuza lakini mwanamke huyo likataa kuondoka akidai, "muungu wa utajiri ni dada yangu.

Tuna mapatano ya kuishi pamoja; unaponifukuza ni lazima afuatane nami." Ni kweli kabisa yule mwanamke mwenye sura mbaya alipotoka nje na mrembo akatoweka.

Kuzaliwa huambatana na kufa. Bahati hufuatana na balaa. Mambo mabaya huambatana na mambo mazuri. Watu yawapasa watambue mambo haya. Wajinga huogopa mikasa na hukazana kupata bahati njema, lakini wao wautafutao Wongofu yawapasa kuepukana na yote na kuwa katika dunia ya mapendo.

12. Zama zile alikuwepo fundi fukara aliyeacha mji wake na mke wake kwenda kutafuta bahati. Baada ya miaka 3 ya kazi ngumu alijipatia vipande mia tatu vya dhahabu na akaamua kurudi nyumbani kwake. Akiwa njiani aliwakuta watu kwenye sikukuu ya kutoa sadaka katika hekalu kubwa. Hii ilimfurahisha sana na akajishauri, "Hadi leo, nimeyawazia mambo ya sasa, sijawazia juu ya furaha ya baadaye hata siku moja. Ni sehemu ya furaha yangu kuwa nimefika mahali hapa; yanipasa nitumie bahati hii kupanda mbegu za matumaini." Akitawaliwa na fikra hizo kwa furaha alitoa akiba yake yote hekaluni na kurudi nyumbani kwake bila senti yoyote.

Alipofika nyumbani kwake mke wake alimsuta kwa kutomletea msaada wowote wa fedha. Fundi fukara alimjibu kuwa alikuwa amepata fedha lakini ameiweka mahali penye usalama. Alipobanwa zaidi aeleze alipoficha hiyo fedha alikiri kuwa alikuwa amewapatia watawa katika hekalu fulani.

Jambo hili lilimkasirisha mke akambeza mume wake na hatima yake akapeleka shauri lake kwa hakimu. Hakimu alipotamka bwana fundi ajitetee, alisema kuwa hakufanya jambo la kijinga kwa kuwa alikuwa amejipatia fedha zake kutokana na mapambano magumu na alihitaji kuitumia kama mbegu ya bahati njema ijayo. Alipofika hekaluni ilielekea kwake kuwa ndicho kiwanja ambapo angepanda dhahabu yake kama mbegu yake ya bahati nasibu. Akaendelea kusema: "Nilipowapatia watawa dhahabu yangu ilikuwa kana kwamba nilitupilia mbali uchoyo na ubahili wote kutoka moyoni mwangu, na nimetambua kuwa utajiri halisi siyo dhahabu bali moyo."

Hakimu alisifu sana roho ya fundi huyo na wale wote waliosikia waliunga mkono kwa kujitolea kwa njia mbalimbali. Hivyo fundi na mke wake waliingia katika bahati njema ya milele.

13. Mtu aliyeishi karibu na makaburini siku moja alisikia sauti ikimwita kutoka makaburini. Alikuwa mwoga kuichunguza sauti hiyo yeye mwenyewe lakini kesho yake alimweleza jasiri rafiki yake, ambaye aliazimia kufuatilia sauti hiyo inapotoka mara sauti hiyo itakaposikika tena usiku ufuatao.

Wakati yule mwoga alipokuwa anatetemeka kwa woga, rafiki yake alikwenda hadi makaburini, na kwa hakika sauti ilisikika kutoka kaburini. Rafiki yake aliuliza ni nani na anataka nini. Sauti toka kuzimuni ilijibu. "mimi ni hazina iliyofichwa ambaye nimeamua kujitoa kwa mtu yeyote. Nilijitoa kwa bwana

mmoja usiku wa jana lakini alikuwa mwoga kufuatilia, kwa hiyo nitajitoa kwako anayeistahili. Kesho asubuhi nitafika nyumbani kwako na wafuasi wangu saba."

Rafiki yake alisema. "Nitakusubiri lakini tafadhali nieleze jinsi ya kukuhudumia" Sauti ilijibu. "Tutakuja tumevaa majoho ya watawa. Andaa chumba chenye maji; oga mwili wako na usafishe chumba, tuwekee viti na bakuli nane za uji wa mchele. Baada ya mlo utatuongoza mmoja mmoja katika chumba kilichofungwa ambapo tutageuka kuwa mitungi ya dhahabu."

Siku iliyofuata asubuhi yake bwana huyo alioga na kusafisha chumba kama alivyoagizwa akabaki akiwasubiri hao watawa wanne. Watawa hao waliwasili kwake na akawapokea kwa ukarimu. Baada ya chakula chao aliwaelekeza kwenye chumba kilichofungwa ambako kila mtawa alijigeuza kuwa mtungi uliojaa dhahabu. Kulikuwa na mtu mwenye choyo sana katika kijiji kilekile aliyesikia tukio hilo akahitaji naye mitungi ya dhahabu. Aliwakaribisha watawa wanne nyumbani kwake. Baada ya chakula aliwaelekeza kwenye chumba kilichofungwa, lakini badala ya kugeuka kuwa mitungi ya dhahabu walikasirika na kuwa wakali kisha wakatoa taarifa polisi ambao walifika kumkamata.

Naye yule mwoga alipopata habari kuwa ile sauti toka kaburini ilimpatia utajiri rafiki yake jasiri, alikwenda kwa rafiki yake na kwa uroho akadai kuwa dhahabu ilikuwa yake kwa kuwa sauti ilimwita kwanza yeye. Mwoga yule alipojaribu kuchukuwa

mitungi alikumbana na nyoka wengi wametokeza vichwa vyao tayari kumshambulia.

Mfalme aliposikia habari hii alitoa hukumu kuwa mitungi ilikuwa mali ya mtu jasiri na akasema: "Kila jambo ulimwenguni huenda hivi. Wajinga wana tamaa ya matukio mazuri tu, lakini ni woga sana kuyafuatilia, na kwa hiyo hushindwa kila mara. Hawana imani wala ushujaa kupambana na migongano ya ndani ya moyo na utulivu wa kweli."

SURA YA PILI

# NJIA YA KUFAIDIKA KWA VITENDO

## I
## KUTAFUTA UKWELI

1. Katika kutafuta kweli kuna baadhi ya maswali yasiyokuwa ya muhimu. Ulimwengu umeumbwa na nini? Ni kwa njia zipi jamii za binadamu zimewekwa pamoja? Ni muundo au sura ipi ya uongozi ulio bora wa jamii ya binadamu? Ikiwa binadamu angeahirisha kutafuta na kutenda matendo ya Wongofu hadi hapo majibu ya maswali hayo yapatikane, angekufa kabla ya kugundua njia.

Fikiria mtu amechomwa na mshale wenye sumu, na ndugu zake na marafiki wamepata kumfuata daktari ili amtoe mshale na kutibu jeraha.

Ikiwa mtu aliyejeruhiwa atapinga akisema, "Subiri kidogo. Kabla ya kutoa mshale, nataka kujua aliyenichoma. Alikuwa mwanamke au mwanaume? Alikuwa mtu wa nasaba bora au mkulima? Uta umetengenezwa na nini? Upinde uliotumika ulikuwa mdogo au mkubwa? Ulikuwa umetengenezwa kwa mti au mwanzi? Kamba ya upinde ilitengenezwa na nini? Ilikuwa imetengenezwa kwa uzi, henzirani au matete? Ni manyoya gani yalitumika? Kabla hamjachomoa mshale nataka kujua yote haya. "Nini basi kitakachofuata?

**Njia ya kufaidika kwa vitendo**

Kabla ya taarifa yote hiyo haijapatikana, bila shaka sumu itakuwa imepata muda wa kusambaa katika sehemu zote za mwili na huenda huyo mtu akafariki. Kazi ya kwanza ni kuondoa mshale na kuzuia sumu isisambae mwilini.

Wakati moto wa mateso unahatarisha ulimwengu, umbile la dunia halina maana ya msingi, upi ni muundo au umbo lipi ni sahihi la jumuiya ya watu vilevile hiyo haina umuhimu wa kuihangaikia.

Kujiuliza juu ya ulimwengu kuwa na mipaka au kuwa ni wa milele kunaweza kusubiri hadi njia itakapopatikana ya kuzima mioto ya kuzaa, uzu, ugonjwa na kifo; katika hali ya taabu, huzuni, maumivu na mateso, mtu yampasa kwanza kutafuta njia ya kutatua matatizo haya na kujitolea kuishika na kuitafuta njia hiyo.

Mafundisho ya Buddha yanahusu mambo yaliyo muhimu kuyajua wala si yale yasiyo muhimu. Hii ina maana watu hawana budi kujifunza wanayopaswa kujifunza, waondoe wanachopasa kuondoa, wajizoeze yale watakayowaongoza.

Kwa hiyo watu yawapasa kuamua yapi ni muhimu, yapi yatatuliwe kwanza na ni jambo lipi lenye shinikizo kwao. Kufanya haya yote yawapasa kujibidiisha kuifunza mioyo yao; kupata kwanza uwezo wa kuitawala mioyo.

2. Kwa mfano mtu anakwenda msituni kutafuta roho iotayo

katikati ndani ya mti na anaporudi anarudi na mzigo wa matawi na majani akidhania kuwa amepata alichokiendea. Je, hatakuwa mjinga akitosheka na gome au ubao badala ya roho ya mti aliyokusudia kupata? Lakini hayo ndiyo wafanyayo watu.

Mtu hutafuta njia itakayomwepusha na uzazi, uzee, maradhi na kifo au taabu, huzuni, maumivu na mateso: na badala yake anafuata njia hiyo kwa muda, anagundua mafanikio kidogo, na mara moja anaanza kujivuna na kudeka kabisa. Mtu huyu naye anakuwa sawa na aliyekwenda msituni kutafuta roho ya mti na akiridhika kwa kurudi nyumbani na mzigo wa matawi na majani.

Mtu mwingine akiwa ametosheka kwa maendeleo yake aliyoyapata kwa juhudi zake kidogo, hupunguza nguvu zake na huanza kujivuna na kuwa na kiburi; amebeba tu mzigo wa matawi na majani badala ya roho ya mti aliyokusudia kupata.

Mtu mwingine pia anapogundua kuwa moyo wake umetulia na mawazo yake yanakuwa wazi, anapunguza juhudi yake na kuanza kujivuna na kuwa na kiburi; ana mzigo wa magome ya miti na wala siyo roho ya mti aliyokuwa akiitafuta.

Basi tena, mtu mwingine huwa na majivuno na kiburi kwa sababu amegundua anayo busara ya kutosha;ana mzigo wa nyuzi za miti badala ya roho ya mti. Watafutaji wote hawa wanatosheka kwa urahisi kwa juhudi zao kidogo na huanza kujivuna na kujitegemea; hupunguza juhudi zao na huanguka katika ulegevu. Watu wote hawa hatimaye watakumbwa na mateso tena.

**Njia ya kufaidika kwa vitendo**

Wale wote waitafutayo njia ya kweli ya Wongofu wasitegemee tuzo ya heshima, utukufu au upendo. Tena wasiende kwa nguvu kidogo, kwa hatua za kipumbavu katika utulivu, maarifa au busara.

Kwanza kabisa yampasa mtu kuelewa kabisa moyoni mwake hali halisi na ya msingi ya ulimwengu wa maisha na kifo.

3. Ulimwengu hauna asili ya pekee. Ni upatanifu mkubwa kwa sababu na hali ya maumbile yenye asili yake tu katika matendo ya moyo ambayo yameshawishiwa na ujinga, fikra potovu, tamaa na ghururi. Sio kitu cha nje ambacho moyo una fikira potofu juu yake ; haina hakika ya pekee kwa hali yoyote ulimwengu umejitokeza kwa mifumo ya akili yenyewe ikidhihirisha madanganyo yake. Imeanzishwa na kujengwa kutokana na tamaa za moyo, kutokana na maumivu, mateso na mapambano yaliyoibuka kutokana na maumivu yaliyosababishwa na uchoyo, hasira na ujinga. Watu wote waitafutayo njia ya Uongofu hawana budi kupambana na roho ya namna hiyo ili waweze kufanikisha malengo yao.

4. " Loh, Moyo wangu! Kwa nini unatangatanga bila kutulia juu ya hali ya mabadiliko ya maisha? Kwa nini unanifanya nichanganyikiwe nisiweze kutulia? Kwa nini unanihimiza nikusanye mambo mengi? Unafanana na plau inayovunjika kabla ya kuanza kulima; unafanana na usukani unaovunjika wakati unatarajia kuvinjari katika bahari ya kufa na kupona. Mageuzi yangu yana maana gani kama hatuwezi kufaidi maisha haya?

" Loh Moyo wangu! Ulinifanya nizaliwe kama Mfalme, halafu ukanifanya nizaliwe kama masikini na niishi kwa kuombaomba. Agharabu umenisababisha nizaliwe katika majumba makubwa ya miungu mbinguni na kuishi katika furaha na anasa; mwisho unanitupia katika tanuru la jehanam.

" Loh Moyo wangu! mjinga! Hivyo umenielekeza katika njia mbalimbali na nimekuwa mtiifu na mtulivu kwako. Lakini kwa kuwa sasa nimesikia mafundisho ya Buddha, usinisumbue tena wala kunifanya niendelee na mateso; bali kwa pamoja tuutafute Uongofu kwa unyenyekevu na utulivu.

" Oh Moyo wangu! Laiti ungejifunza kuwa kila kitu hakina hakika na ni cha kupita; kama ungejifunza kutoshikilia mambo, kutotamani vitu, kutotoa nafasi kwa choyo, hasira na ujinga; bila shaka tungeweza kusafiri katika utulivu. Basi kwa kuvunjavunja pingu na kamba za tamaa kwa sime ya hekima, bila ya kubughudhiwa na manzili yabadilikayo-faida au hasara au baya, baraka au balaa, sifa au bezo-huenda tukaishi kwa amani.

" Oh, moyo wangu mpendwa! Ni wewe uliyeamsha imani ndani yetu; ni wewe uliyetushauri kuutafuta Uongofu. Kwa nini unarahisika tena kufungua milango kwa choyo; kwa mapenzi ya starehe na mahangaiko.

" Oh, moyo wangu, kwa nini unahangaika hapa na pale bila dhumuni mahsusi? Hebu tuvuke hii bahari kubwa ya madanganyo. Hadi sasa nimekuwa nikitenda kama upendavyo na

kwa pamoja tutafuata mafundisho ya Buddha.

" Oh, moyo wangu mpendwa! Hii milima, mito, na bahari inabadilika na inasababisha maumivu. Ni wapi katika dunia hii ya madanganyo tutakapopata utulivu? Hebu tufuate mafundisho ya Buddha na tuvuke hadi pwani nyingine ya Wongofu."

5. Kwa hiyo wale waitafutao njia ya Nuru hasa huamrisha mioyo yao. Kisha huendelea kwa azma kuu. Ingawa wanatukanwa na kusutwa na baadhi ya watu, wanasonga mbele bila kukata tamaa . Hawakasiriki wanapopigwa ngumi au mawe au wanapokatwa mapanga.

Hata kama maadui watakata vichwa vyao na kuacha viwiliwili, moyo usihangaike. Wakiruhusu mioyo yao ifunikwe na mambo yawaumizayo, hawafuati mafundisho ya Buddha. Yawabidi kukata shauri bila kujali litakalowatokea, kusimama imara, bila kuyumba daima wakisambaza fikra na mawazo ya huruma na ukarimu. Wacha matusi yaje, wacha balaa ije na bado mtu haitambidi kutoyumbayumba bali moyoni kubaki amejaa mafundisho ya Buddha.

Kwa nia ya kuupata Wongofu, yampasa mtu kujaribu kukamilisha yasiyowezekana, kustahimili yasiyostahimilika. Yampasa mtu kutoa yote aliyo nayo. Ikiwa mtu ataambiwa kuwa ili kuupata Uongofu inabidi apunguze chakula chake hadi punje moja ya mchele kila siku, atakula punje moja tu. Ikiwa njia ya Uongofu inapitia motoni mtu atasonga mbele.

Lakini mtu asifanye haya yote kwa madhumuni ya kutenda kinyume. Mtu atende itakiwavyo kwa sababu ni jambo la busara na sahihi. Mtu atende mambo hayo kutokana na roho ya huruma kama mama amfanyiavyo mtoto wake mchanga, kwa mtoto wake mgonjwa, bila kuwazia nguvu zake au faraja.

6. Zama za kale alikuwepo mfalme aliyependa nchi yake na watu wake na aliwatawala kwa hekima na huruma na matokeo yake nchi hiyo ilipata maendeleo makubwa na amani. Kila mara alijitahidi kuongeza hekima yake na elimu; Wakati mwingine alitoa zawadi kwa mtu yeyote aliyeweza kumpa mafundisho ya busara.

Hekima na bidii yake hatimaye viliwafikia miungu walioapa kumjaribu. Muungu alijigeuza kuwa jini, akaenda langoni kwa Mfalme akaomba aonane naye ili ampatie mafundisho matakatifu.

Naye Mfalme aliyefurahia kusikia taarifa hiyo alilikaribisha jini hilo vizuri limpe mafundisho. Jini lilibadilika katika sura ya kutisha na likadai lipewe chakula linachotaka kabla ya kutoa mafundisho. Chakula kilipoletwa jini lilidai lipewe nyama na damu ya binadamu ambayo bado ina moto. Mwana wa Mfalme na malkia walitoa miili yao likawala lakini jini hilo halikuridhika hivyo likadai mwili wa Mfalme.

Mfalme alijiweka tayari kutoa mwili wake ila akadai asikie fundisho kwanza kabla ya kuutoa mwili wake.

Muungu alitoa fundisho la busara lifuatalo: Taabu hutokana na tamaa na woga hutokana na tamaa. Wale walioachana na tamaa hawana taabu wala woga." Mara moja Muungu akarudia sura yake na mwana wa Mfalme pamoja na malkia wakatokea katika maumbo yao.

7. Hapo kale kulikuwa na mtu aliyeitafuta Njia ya kweli ya kwenda Himalaya. Hakufikiria lolote kuhusu hazina ya duniani ama furaha za ahera bali alitafuta mafundisho yatakayomwondolea madanganyo akilini mwake.

Miungu walifurahishwa na bidii na unyofu wa mtu huyo na wakaamua kujaribu moyo wake. Hivyo mmoja wa miungu alijigeuza kuwa jini na akajitokeza katika milima ya Himalaya, akiimba: " Kila kitu hubadilika, kila kitu hutokea na kupotea."

Mtafutaji alipousikia wimbo huu alifurahi sana. Alijiwa na furaha kuu kana kwamba amepata kisima cha maji kwa kiu yake ama kama mtumwa aliyeachiwa huru bila ya kutarajia. Alijisemea, "sasa nimepata mafundisho ya kweli niliyokuwa nikitafuta kwa muda mrefu." Aliifuatilia sauti hadi alipofikia jini lenye sura ya kutisha. Kwa moyo wa wasi wasi aliliendea lile jini na kusema "je, ni wewe uliyeimba wimbo mtakatifu niliousikia? Kama ni wewe tafadhali endelea kuimba."

Jini lilijibu:" Ndiyo, ulikuwa wimbo wangu, lakini siwezi kuuendeleza hadi nitakapokuwa nimepata chakula; ninakufa kwa njaa."

Bwana huyo alimsihi sana kwa bidii aendelee kuimba, akisema, "Wimbo huo una maana takatifu kwangu na nimetafuta mafundisho yake kwa muda mrefu. Nimesikia sehemu yake tu; tafadhali niruhusu nisikie ziada yake."

Jini lilisema tena: Ninakufa kwa njaa lakini nikionja nyama mbichi ya binadamu na damu yake nitaumalizia wimbo."

Kwa kuwa mtu huyo alikuwa na nia ya kusikia mafundisho aliahidi kutoa mwili wake kwa jini baada ya kusikia mafundisho. Hapo jini liliimba wimbo wote.

Kila kitu hubadilika,
Kila kitu huonekana na kutoweka,
Kuna uhuru wa kweli,
Mtu anaposhinda maisha na kifo.

Baada ya kulisikia shairi hilo yule mtu aliliandika kwenye miamba na miti kisha akapanda juu ya mti ajitupe chini ya miguu ya jini, lakini wakati huo jini lilishatoweka na badala yake muungu aliyejaa furaha alimpokea bila kuumia.

8. Hapo kale kulikuwa na mtu mwenye bidii ya kutafuta njia ya kweli aliyeitwa Sadaprarudita. Alitupilia mbali majaribio yote kwa faida au heshima na kuitafuta njia kwa kujitolea maisha yake. Siku moja alisikia sauti kutoka mbinguni ikisema, "Sadaprarudita! "Ondoka hapa uelekee Mashariki usifikirie joto au baridi, usijali sifa za kidunia wala bezo, usibughudhiwe na tofauti ya mema na

maovu ila kaza mwendo mbali utapata mwalimu wa kweli nawe utapata Uongofu."

Sadaprarudita alifurahi sana alipopata maelekezo ya hakika na akaondoka mara moja kuelekea Mashariki. Agharabu alilala popote pale, nyikani au milimani.

Akiwa mgeni katika nchi ya ugenini alipata maudhi mengi; Wakati fulani alijiuza utumwani, aliuza mwili wake kwa sababu ya njaa, lakini mwisho alipata mwalimu wa kweli akamwomba maelekezo.

Kuna methali isemayo " Vitu vizuri ni ghali" na Sadaprarudita alithibisha ukweli huu kwa kuwa alikumbana na vipingamizi vingi katika kutafuta njia.

Hakuwa na fedha yoyote ya kununulia maua na ubani wa kumpatia mwalimu. Alijitahidi kuuza huduma zake lakini mtu wa kumkodisha hakupatikana. Ilielekea kulikuwa na pepo mbaya akimkwamisha katika njia yoyote aliyojaribu. Njia ya kuelekea kwenye Uongofu ni ngumu inaweza kupoteza maisha ya mtu.

Mwisho Sandaprarudita alifika mahali alipokuwa mwalimu ila akawa na tatizo jipya. Hakuwa na karatasi wala wino au brashi ya kuandikia. Hivyo alichoma mkono wake kwa sime na akaandika kwa kutumia damu yake. Kwa njia hii alifaulu kuipata kweli ya thamani.

9. Zama zile kulikuwa na mvulana, jina lake Sudhana ambaye pia alihitaji Uongofu na kwa bidii aliitafuta njia. Kutokana na mvuvi alijifunza elimu ya bahari. Kutoka kwa daktari alijifunza huruma kwa wagonjwa katika maumivu yao. Kwa tajiri alijifunza kuwa kuweka akiba ya fedha ndiyo ilikuwa siri ya bahati yake na akapata wazo kuwa ni lazima kuweka akiba ya kila kitu kilichopatikana katika njia ya Uongofu.

Kutokana kwa mtawa anayetafakari alijifunza kuwa moyo safi na wa imani una nguvu za kimiujiza za kusafisha na kutuliza mioyo mingine. Siku moja alikutana na mwanamke wa haiba ya hali ya juu na akavutiwa na roho yake ya ukarimu na kutokana naye akajifunza kuwa hisani ni matunda ya hekima. Siku nyingine alikutana na mtembezi mmoja wa makamo aliyemwambia kuwa kufika mahali fulani itambidi apande mlima wa mapanga na kupitia katika bonde la moto. Kwa hiyo alijifunza kutokana na uzoefu wake kuwa kulikuwa na fundisho kutokana na kila kitu alichokiona au alichosikia.

Alijifunza uvumilivu kutoka kwa mwanamke kiwete, maskini; alijifunza somo la furaha isiyo na gharama kwa kuangalia watoto wakicheza barabarani; na kutoka kwa watu waungwana na wanyenyekevu, ambao hawakufikiwa kuhitaji jambo lolote litakiwalo na watu wengine, alijifunza siri ya kuishi kwa amani na ulimwengu wote.

Kutokana na kuangalia mchanganyiko wa sehemu za ubani alijifunza somo la mapatano, na kutokana na mpangilio wa maua

alijifunza somo la sadaka na shukrani. Siku moja alipokuwa akipita msituni, alijipumzisha chini ya mti bora na akaona mche mdogo ukiota karibu kutokana na mti ulioanguka pale ukaoza na akajifunza somo la maisha kutokuwa na uhakika.

Mwanga wa jua na kumetameta kwa nyota, mara kwa mara vilimburudisha sana. Kwa hiyo Sudhana alifaidika kutokana na uzoefu wa safari ndefu.

Hakika wale waitafutao Nuru Kuu yawapasa wafikirie mioyo yao kama ngome na waipambe. Yawabidi pia wafungue malango ya mioyo yao kwa Buddha, na kwa heshima na unyenyekevu wamkaribishe ili aingie katika mwandani wao ili wakamtolee yeye ubani wenye manukato ya imani na maua ya furaha na shangwe.

## II
## NJIA ZA MATENDO

1. Kwa wale waifuatao Nuru kuna njia tatu za utendaji ambazo zinapaswa kueleweka na kufuatwa: kwanza, taratibu ya tabia za utendaji; pili utulivu sahihi wa moyo; na tatu, hekima.

Taratibu ni zipi? Kila mmoja awe ni mlalahoi au mtafutaji wa njia, lazima afuate mafundisho kwa tabia nzuri. Lazima atawale vyote moyo na mwili wake, na alinde milango ya fahamu zake sita. Nilazima aogope hata ovu dogo, na mara kwa mara ajitahidi

kutenda matendo mema tu.

Utulivu wa moyo una maana gani? Una maana ya kuondokana haraka na uchoyo na tamaa mbaya zinapojitokeza, na kutunza moyo kwa usafi na utulivu.

Hekima ni nini? Ni uwezo wa kutambua kwa usahihi na kukubali kwa utaratibu wa ukweli bora, kujua chanzo cha mateso, kinachofanya mwisho wa mateso.

Wale wafuatao njia hizi tatu za utendaji kwa bidii wana haki ya kuitwa mitume wa Buddha.

Fikiria punda, ambaye hana umbo zuri, hana sauti wala pembe kama zile za ng'ombe anafuata kundi  la ng'ombe na akitangaza, " Tazama mimi pia ni ng'ombe. "Je kuna mtu atakayemwamini? Ni ujinga mtupu pia mtu anaposhindwa kufuata njia tatu za utendaji lakini anapotakabari kuwa yeye ni mtafutaji wa njia, ama mtume wa Buddha.

Kabla ya mkulima hajakusanya mavuno inabidi kwanza alime ardhi, apande mbegu, amwagilie na apalilie magugu wakati wa masika. Vilevile, mtafutaji wa wongofu lazima afuate njia tatu za utendaji. Mkulima hawezi kutegemea kuona mbegu zinaota leo, kuona mimea kesho, na kukusanya mazao kesho kutwa. Kwa hiyo mtu aitafutaye Nuru hawezi kutegemea kuachana na tamaa mbaya kesho yake na kuipata Nuru kesho kutwa.

**Njia ya kufaidika kwa vitendo**

Kama mimea inayopata utunzaji bora kutoka kwa mkulima tangu mbegu inapopandwa na wakati wa kubadilika kwa hali ya hewa hata wakati wa kukua toka kuota hadi kutoa matunda, hivyo basi mtafutaji wa Uongofu ni lazima alime na kutifua udongo wa Uongofu kwa bidii na ustahimilivu kwa kufuata njia tatu za utendaji.

2. Ni vigumu sana kuendelea kufuata njia na starehe, na moyo ukisumbuliwa na tamaa za milango ya fahamu. Kuna tofauti kati ya starehe ya maisha na starehe ya Njia ya Kweli.

Kama ilivyokwisha elezwa, moyo ndiyo chanzo cha mambo yote. Moyo unapopenda mambo ya kidunia, madanganyo na mateso bila shaka, vitafuata, lakini moyo unapopenda na kufurahia Njia ya kweli, hakika furaha na mafundisho vitafuata.

Kwa hiyo watu wafuatao Uongofu yawapasa kuwa na mioyo safi na kwa uvumilivu wafuate njia tatu za utendaji. Ikiwa wafuasi watafuata mafundisho, kwa kawaida watapata utulivu wa moyo; na ikiwa watapata utulivu wa moyo itakuwa jambo la kawaida kwao kupata hekima, na hekima hiyo itawaelekeza kwenye Uongofu.

Kwa hakika hizi njia tatu(kufuata mafundisho, kushika utulivu wa moyo, na kila mara kufanya mambo kwa busara) ni njia za kweli za kuelekea kwenye Nuru.

Kwa kutozifuata hizo njia tatu, kwa muda mrefu watu wanakusanya madanganyo ya akili. Wasibishane na watu wa duniani, bali, kwa utaratibu na uvumilivu watafakari undani wa dunia yao ya moyo safi kuupata Uongofu.

3. Ikiwa njia tatu za utendaji zitachambuliwa, zitadhihirisha njia nane bora, mitizamo minne ya kufikiriwa, taratibu nne sahihi, vitivo vinne vya nguvu zitakazotumika na ukamilifu wa njia sita za utendaji.

Njia Nane Bora ina maana ya mtizamo sahihi, fikra sahihi, maneno sahihi, tabia sahihi, maisha sahihi, nguvu sahihi, utu sahihi na utulivu sahihi.

Mtizamo Sahihi ina maana ya kuelewa kwa ufasaha U-nne wa Ukweli, kuamini kanuni ya sababu na matokeo na kutokudanganywa na sura na tamaa.

Fikra Sahihi ina maana ya azima ya kutozienzi tamaa, kutokuwa mchoyo, kutokasirika na kutofanya jambo lolote la kudhuru

Maneno Sahihi maana yake ni kuepuka kusema uwongo, kuseng'enya, kutukana na kutokuwa kidhabidhabina.

Tabia sahihi ina maana ya kujiepusha na maisha yanayoweza kuleta aibu.

**Njia ya kufaidika kwa vitendo**

Nguvu Sahihi ina maana ya kujitahidi kwa uangalifu kufuata uelekeo sahihi.

Utu Sahihi ina maana kuwa na moyo ulio safi na wenye akili na mawazo mema.

Utulivu sahihi ina maana ya kuuweka moyo katika hali iliyo huru kuuwezesha kutulia, ili kupata utakaso halisi wa moyo.

4. Mitizamo minne ya kufikiria ni: kwanza kufikiria mwili kuwa mchafu, kujitahidi kuondoa mapendo yote kwake, pili kufikiria milango ya fahamu kama chimbuko la mateso bila kujali hisia zake za furaha au maumivu; tatu, kuufikiria moyo kuwa katika hali ya kutiririka daima, na nne, kufikiria kuwa kila mtu duniani ni matokeo ya sababu na hali ya maumbile na hakuna kitu kisichobadilika milele.

5. Taratibu nne sahihi ni: Kwanza ni kuzuia uovu wowote usitokee: pili kuondoa uovu wowote unapotokea; tatu ni kushawishi utendaji wa matendo mema, na nne ni kutia moyo ukuzaji na ustawishaji wa matendo mema yaliyokwisha jitokeza. Kila mtu yampasa ajitahidi kufuata taratibu hizi nne.

6. Misingi mitano ya nguvu ni: Kwanza ni Imani ya kuamini; pili ni nia ya kujitahidi; tatu ni msingi wa kusimama kidete; nne ni uwezo wa kutuliza moyo; na tano ni uwezo wa kulinda hekima safi. Misingi hii mitano ni nguvu za lazima ili kuupata Wongofu.

7. Ukamilifu wa mazoezi sita ya kufikia ukingo mwingine wa Nuru ni: njia ya matoleo na sadaka, njia ya kutunza mafundisho, njia ya utulivu wa moyo, na njia ya hekima. Kwa kufuata njia hizi, hakika mtu atavuka kutoka ukingo wa madanganyo kwenda ukingo wa Nuru.

Zoezi la matoleo linaondoa uchoyo; Zoezi la Mafundisho humfanya mtu afikirie haki na raha za wengine; Zoezi la uvumilivu humsaidia mtu kutawala moyo ulio hafifu na unaotangatanga; na zoezi la Hekima huubadilisha moyo uliochanganyikiwa na uliojaa giza katika moyo wa busara safi.

Matoleo na kushika Mafundisho hujenga msingi madhubuti ambao ni wa lazima kujengea ngome juu yake. Uvumilivu na Bidii ni kuta za kuizuia ngome isishambuliwe na maadui kutoka nje. Utulivu na Hekima ni silaha za kujilinda kutokana na mashambulizi ya maisha na kifo.

Ikiwa mtu hutoa zawadi pale inapowezekana au kwa vile ni rahisi kutoa kuliko kutokutoa, hayo ni Matoleo, lakini siyo Matoleo ya kweli. Matoleo ya kweli hutokana na moyo wa huruma kabla ya ombi lolote na Matoleo ya Kweli hutolewa mara kwa mara wala siyo kwa msimu.

Wala hayatakuwa Matoleo ya Kweli ikiwa baada ya tendo hilo kutazuka hisia za kujilaumu au kujitukuza; Matoleo ya Kweli ni yale yatolewayo kwa furaha, kwa kujisahau kama mfadhili (mtoaji) kama mpokeaji, na zawadi yenyewe.

**Njia ya kufaidika kwa vitendo**

Matoleo ya kweli hutoka bila kusudio la kupangwa kutoka kwa moyo wenye huruma, bila matumaini ya kulipwa au kurudishiwa fadhila ukitegemea kuingia pamoja katika Uongofu.

Kuna aina saba za matoleo ambazo zinaweza kutendwa hata na watu wasio matajiri. Ya kwanza ni matoleo ya nguvu. Huku ni kutoa huduma kwa kufanya kazi. Aina ya juu sana ya Matoleo haya ni mtu kujitoa maisha yake kama inavyoonekana katika hadithi ifuatayo: ya pili ni matoleo ya kiroho. Ya tatu ni matoleo ya macho. Hii ni kutoa mtizamo wa ukarimu. Ya nne ni matoleo ya wajihi. Hii ni kutoa uso laini na wa tabasamu kwa wengine. Ya tano ni matoleo ya kauli. Hii ni kutoa maneno ya upole. Ya sita ni matoleo ya kiti. Hii ni mtu kutoa kiti chake kwa wengine. Ya saba ni matoleo ya nyumba. Hii ni kuwakaribisha watu wengine kulala nyumbani kwake. Aina hizi za matoleo zinaweza kutolewa na mtu yeyote katika maisha ya kila siku.

8. Zama zile kulikuwa na mwana wa mfalme jina lake Sattva. Siku moja yeye na kaka zake walikwenda kucheza msituni. Huko walimwona chui jike aliyekuwa amekabwa na njaa na akishawishika kuwala makinda wake saba.

Kaka zake walikimbia lakini Sattva alipanda juu ya jabari akajiangusha miguuni pa chui jike ili aokoe maisha ya vitoto vya huyo chui.

Sattva, mwana wa Mfalme, alitenda tendo la hisani bila kupanga lakini moyoni mwake alikuwa akifikiri: "Mwili huu

unabadilika na siyo wa kudumu. Nimeupenda mwili huu bila wazo la kuutupa lakini sasa niutoe sadaka kwa chui jike huyu ili nikaupate Uongofu." Wazo hili la mwana wa Mfalme Sattva linaonyesha ujasiri wa kweli wa kupata Uongofu.

9. Kuna Hali Nne zisizo na kikomo za Moyo ambao kwanza mtafutaji wa Nuru anapaswa kuzilinda. Nazo ni huruma; Utu wema, uchangamfu na utulivu. Mtu anaweza kuepukana na hasira kwa utulivu. Mtu anaweza kuepuka tabia ya kuwatofautisha marafiki na maadui kwa kulinda moyo mwadilifu.

Ni huruma kubwa iwafanyao watu wafurahi na kuridhika; ni utu - mwema unaoondoa jambo lolote linalowakosesha watu furaha na kuridhika, ni uchangamfu unaomfanya kila mtu afurahi na kuridhika kwa moyo wa furaha, kuna wingi wa amani kila mtu anapofurahi na kutosheka na mtu anaweza kuwa na hisia sawa kwa kila mtu.

Kwa uangalifu mtu anaweza kulinda hizi Hali nne zisizokuwa na kikomo na akaweza kuondokana na choyo, hasira, mateso na moyo wa upendo-chuki, lakini hilo siyo jambo rahisi kutenda. Ni vigumu kuondoa moyo mwovu kama ilivyo vigumu kumuondoa mbwa kwenye lindo, na ni rahisi kuupoteza moyo sahihi kama kulungu msituni; ama ni vigumu kuuondoa moyo mwovu kama ilivyo vigumu kuyafuta maandishi yaliyoandikwa kwenye mwamba au jiwe, na moyo sahihi ni rahisi kuupoteza kama maandishi yaliyoandikwa kwenye maji. Kwa hakika, ni jambo gumu sana katika maisha mtu kujiongoza ili

kuupata Uongofu.

10. Kulikuwa na kijana mmoja jina lake Srona aliyezaliwa katika familia ya kitajiri lakini mwenye afya hafifu. Alikuwa na bidii ya kuupata Uongofu, akawa mtume wa Aliyebarikiwa. Katika njia ya Nuru alijitahidi hadi miguu yake ikavimba.

Aliyebarikiwa alimwonea huruma akasema "Srona kijana wangu, ulijifunza kinubi nyumbani kwenu? Unajua kuwa kinubi hakiwezi kutoa muziki ikiwa nyuzi zimevutwa sana au zimelegezwa sana? Kinubi kinatoa muziki ikiwa nyuzi zake zimevutwa kwa usahihi.

"Mafundisho ya Wongofu ni kama kurekebisha nyuzi za kinubi. Huwezi kuupata Uongofu ikiwa utavuta sana au kulegeza sana moyo wako. Yakupasa kuwa mwangalifu na mwenye busara."

Srona aligundua kuwa maneno haya yalikuwa ya faida na mwishowe akapata alichokitaka.

11. Zama zile kulikuwa na mwana wa Mfalme ambaye alikuwa bingwa katika matumizi ya silaha tano. Siku moja alipokuwa anatoka kwenye mazoezi alikutana na dubwana ambalo ngozi yake ilikuwa ngumu kupindukia.

Dubwana hilo lilimshambulia lakini mwana wa mfalme hakuogopa katu. Kwanza alilichoma kwa mshale lakini

haukuliumiza popote. Pili alilitupia mkuki lakini ulishindwa kutoboa ngozi yake. Tena alilitupia ufito na Sagai lakini vyote vilishindwa kuipenya ngozi yake. Tena akatumia sime yake lakini haikufaa kitu, kwani dubwana hilo lilimdaka kwa mamikono yake na kumbana kwa nguvu. Basi tena mwana wa mfalme alijitahidi kutumia kichwa chake lakini hakikumsaidia.

Dubwana lilisema " Ni kazi bure wewe kukataa, nitakumeza." Lakini mwana wa mfalme alijibu." Huenda ukafikiri kuwa nimetumia silaha zangu zote hivyo sina msaada wowote, bado nina silaha moja iliyobaki. Ukinimeza nitakuharibu niwapo ndani ya tumbo lako."

Ushupavu wa mwana wa Mfalme ulilibabaisha sana dubwana na likauliza " Unawezaje kufanya hivyo?" Mwana wa mfalme alijibu "Kwa uwezo na nguvu za kweli."

Kisha dubwana lilimwachia na likamwomba alipatie mafundisho juu ya ukweli."

Mafundisho katika hadithi ni kuwatia moyo mitume kuwa na bidii katika harakati zao na kutokuwa na hofu wapambanapo na vikwazo.

12. Tabia ya kukarahisha na kujitanguliza humkwaza binadamu lakini dharau na aibu huwalinda binadamu. Watu huwaheshimu wazazi wao, kaka zao na dada zao kwa sababu ni wepesi wa kutambua dharau na aibu. Baada ya kujichunguza ni jambo la

heshima kujiepusha na utukuzaji wa nafsi na kuona aibu tuwaangaliapo watu wengine.

Ikiwa mtu ana roho ya toba, dhambi zake zitatoweka, lakini kama ana roho asiyokuwa na toba ndani mwake dhambi zake zitaendelea na zitamwangamiza milele.

Ni yule tu ayasikiaye mafundisho ya kweli kwa usahihi na kutambua maana na uhusiano wa mafundisho hayo kwake atakaye yapokea na kufaidika.

Ikiwa mtu atasikia mafundisho ya kweli lakini hayapokei, atashindwa katika juhudi za kuitafuta Nuru.

Imani , adabu, unyenyekevu, bidii na hekima ni misingi ya nguvu kwa yule anayeutafuta Uongofu. Kati ya misingi hiyo, hekima ndiyo kubwa zaidi na mengineyo ni sura za hekima. Kama mtu atapenda mambo ya kidunia, atafurahia kuplga maneno au kulala usingizi, ataiacha njia ya Uongofu.

13. Wakati wa mafundisho ya Uongofu, baadhi ya watu wanafaulu kwa haraka kuliko wenzao. Kwa hiyo mtu asikate tamaa kuwaona wenzake wanatangulia kuongoka.

Mtu anapojifunza ufundi wa kupiga upinde, hategemei kufaulu kwa haraka bali anafahamu kuwa akifanya mazoezi kwa uvumilivu taratibu, atafaulu barabara . Mto huanza kama kijito lakini huendelea kupanuka hadi kutiririka katika bahari kuu.

Kama kwenye mifano hii, ikiwa mtu atajifunza kwa uvumilivu na kwa bidii ataupata Uongofu bila wasiwasi.

Kama ilivyokwisha elezwa, ikiwa mtu atafungua macho yake, atayaona mafundisho kila mahali na hivyo nafasi zake za Uongofu ni nyingi sana.

Wakati fulani kulikuwa na mtu mmoja aliyekuwa anaunguza ubani. Aligundua kuwa harufu ya manukato ilikuwa haiji wala haiendi; haikutokea wala kutoweka. Tukio hilo dogo lilimsaidia kuipata Nuru.

Siku za kale mtu mmoja alichomwa mwiba katika mguu wake. Alipata maumivu makali na wazo likamjia kuwa maumivu yalikuwa yanabainishwa na moyo. kutokana na tukio hilo wazo zito lilimjia kuwa moyo usipotawaliwa unaweza kupotea au unaweza kuwa mtakatifu mtu anapofaulu kuutawala. Kutokana na mawazo hayo baada ya kitambo kidogo, Uongofu ulimjia.

Kulikuwa na mtu mwingine aliyekuwa bahili. Siku moja alikuwa anawazia juu ya moyo wake wa uchoyo alipogundua kuwa mawazo ya uchoyo yalikuwa ni vidonda na takataka ambazo zingeweza kuchomwa na kuteketezwa na hekima. Huo ulikuwa ni mwanzo wa Nuru.

Kuna msemo usemao: "Weka akili yako sawasawa. Ikiwa akili yako iko sawa, dunia yote itakuwa sawa." Fikiria maneno haya. Elewa kuwa tofauti zote duniani zinasababishwa na

mpambanuo wa mawazo ya moyo. Kuna njia ya Nuru katika maneno hayo Hakika njia za Nuru ni nyingi sana.

## III
## NJIA YA IMANI

1. Wale wote wapatao hifadhi katika hazina tatu, Buddha, Dharma na Samgha wanaitwa mitume wa Buddha, hushika na kufuata sehemu nne za utawala -wa- Moyo-mafundisho, imani, matoleo na hekima.

Mitume wa Buddha hushika mafundisho matano: usiibe, usiue, usizini, usiseme uwongo na usinywe kileo cha aina yoyote.

Mitume wa Buddha wana imani katika hekima kamili ya Buddha, Hujitahidi kuepukana na tamaa na uroho na kuitoa sadaka. Wanaifahamu kanuni ya chanzo na matokeo wakiwekea maanani mpito wa maisha na kushika kanuni ya hekima.

Mti unaoegemea mashariki, ukianguka utaangukia Mashariki na vivyo hivyo wale wanaosikiliza mafundisho ya Buddha na kuyaamini hakika watazaliwa katika Nchi Takatifu ya Buddha.

2. Ni hakika ilivyosemwa kuwa watu wanaoamini hazina tatu za Buddha, Dharma na Samgha wanaitwa Mitume ya Buddha.

Buddha ndiye aliyeipata Nuru kamili na alitumia ushindi wake kuwafungua na kuwabariki binadamu wote. Dharma ni Ukweli, roho ya Uongofu na mafundisho yanayoielezea. Samgha ni undugu Sahihi wa waumini katika Buddha na Dharma.

Tunazungumzia u-Buddha, Dharma, Udugu, kana kwamba ni vitu vitatu tofauti, anajidhihirisha katika Dharma na anatambulikana katika Udugu. Kwa hiyo kuamini Dharma na kuuhifadhi udugu ni kuwa na imani katika Buddha, na kuwa na imani katika Buddha ina maanisha kuamini Dharma, kuhifadhi udugu.

Kwa hiyo watu wanaongoka na kuwa huru kwa kuwa na imani tu katika Buddha. Buddha ni Mwongofu wa kweli na Hupenda kila mtu kana kwamba kila mmoja ni mtoto wake wa pekee. Hivyo basi, mtu yeyote anayemtambua Buddha kama mzazi wake, amejitambulisha kwake na atapata Uongofu.

Wale watambuao Buddha watalindwa na hekima yake na kutiwa manukato kwa neema yake.

3. Hakuna kitu chochote duniani kiletacho manufaa kuliko kumwamini Buddha. Kusikia tu jina la Buddha, kuamini na kufurahi angalau kwa kitambo kidogo tu, kuna tuzo isiyokuwa na kifani.

Kwa hiyo mtu hana budi kufurahi kwa kutafuta mafundisho ya Buddha licha ya moto mkubwa ulioijaza dunia

nzima.

Siyo rahisi kukutana na mwalimu anayeweza kuifafanua Dharma; itakuwa vigumu kukutana na Buddha; Lakini itakuwa vigumu zaidi kuyaamini mafundisho yake.

Lakini kwa sasa umekutana na Buddha, ambaye ni vigumu kukutana naye na umeelezwa yale ambayo ni vigumu kusikika, unapaswa kuamini na kufurahi na kuwa na imani katika Buddha.

4. Imani ni mmojawapo wa marafiki aliye bora katika safari ndefu ya maisha ya binadamu; ni kiburudisho bora safarini na ni mali.

Imani ni mkono unaopokea Dharma, ni mkono mtakatifu unaopokea wema wote. Imani ni moto unaozunguka uchafu wote wa tamaa za dunia; inaondoa mzigo, na ni kiongozi aonyeshaye mapito.

Imani huondoa woga, choyo na majivuno, hufundisha ukarimu na kuwaheshimu wengine, humweka mtu huru kutoka katika utumwa wa manzili; humtia hamasa kuweza kupambana na matatizo; humpatia mtu nguvu za kushinda majaribu; humwezesha mtu kutenda matendo mema na matakatifu, na hujaza moyo hekima.

Imani ni faraja wakati njia ya mtu inapokuwa ndefu na ya kuchosha, na huelekea kwenye Nuru.

Imani hufanya tujisikie kuwa pamoja na Buddha na hutuleta pale mkono wa Buddha unapotushikilia. Imani huilainisha mioyo migumu na ya uroho na hutupa roho ya upendo na moyo wa kuelewa utu wema na huruma.

5. Watu wenye imani hupata hekima kutambua mafundisho ya Buddha kwa lolote wanalolisikia. Wale wenye imani hupata hekima ya kuona kuwa kila kitu si kingine bali ni uwepo ambao unatokana na kanuni ya sababu na hali ya maumbile, na tena imani huwapa unafuu wa kupokea kwa uvumilivu na uwezo wa kukubaliana na hali zao kwa amani.

Imani huwapa hekima ya kutambua mpito wa maisha na neema yakutoshtushwa au kusikitishwa na lolote linalowatokea au kwa maisha yenyewe yapitayo wakijua kuwa hata hali na maumbo vitabadilika, ukweli wa maisha daima kubakia bila kubadilika.

Imani inazo sura muhimu tatu: toba, heshima ya furaha na ukweli kwa wema wa watu wengine, na ukubali upeo wa kuwepo kwa Buddha.

Watu hawana budi kustawisha sura hizi za imani; yawapasa kuwa wepesi wa kuona kushindwa kwao na uchafu; yawapasa kuyaonea aibu na kutubu; yawapasa kujifunza kutambua tabia nzuri; matendo mema ya wengine na kuyapa sifa; pia yawapasa kila mara kutamani kutenda na kuishi na Buddha.

**Njia ya kufaidika kwa vitendo**

Moyo wa imani ni moyo wa ukweli; ni moyo wenye fikra nzito, moyo ambao umejaa uchangamfu wa kweli kuelekea katika Nchi Takatifu ya Buddha kwa Nguvu zake.

Kwa hiyo, Buddha huipa nguvu imani ambayo huwaongo za watu katika Nchi Takatifu, nguvu ambayo huwatakasa, nguvu ambayo huwalinda kutokana na madanganyo ya nafsi zao. Hata kama wameipokea imani kwa kitambo tu, walisikiapo neno lake Buddha likisifiwa duniani kote, wataelekea katika Nchi Takatifu.

6. Imani siyo kitu kinachoongezewa katika moyo wa kidunia, ni ya asili ya Buddha iliyomo ndani ya moyo. Yeyote amwelewaye Buddha naye ni Buddha, yeyote mwenye imani katika Buddha amekuwa Buddha.

Lakini ni vigumu kuitafuta na kuipata asili ya Buddha ya mtu, ni vigumu kutunza moyo mtakatifu katika mabadiliko ya kila mara ya choyo, hasira na mateso ya dunia; bali imani humwezesha mtu kutenda yote hayo.

Katika msitu wa miti ya Eranda yenye sumu, ni miti ya Eranda yenye sumu tu iotayo humo wala siyo miti ya Chandana yenye matunda matamu na ya harufu nzuri za manukato. Ni muujiza ikiwa miti ya Chandana itaota na kustawi ndani ya misitu ya Eranda. Vivyo hivyo ni muujiza, imani katika Buddha kuota na kustawi ndani ya moyo wa watu.

Kwa hiyo, imani ya kumwamini Buddha inaitwa "imani isiyo na mizizi" yaani haina mizizi ya kuota kwenye mioyo ya binadamu bali ina mizizi ya kustawi katika moyo wa huruma wa Buddha.

7. Hivyo basi, imani ni takatifu na huzaa matunda. Bali ni vigumu kuamsha imani katika moyo mlegevu. Kwa usahihi, kuna mashaka matano ambayo hujificha katika vivuli vya moyo wa binadamu na hujitahidi kuikatisha imani tamaa.

Kwanza kuna mashaka katika hekima ya Buddha, pili kuna mashaka katika mafundisho ya Buddha; tatu kuna mashaka juu ya mtu anayeelezea mafundisho juu ya Buddha, nne kuna mashaka juu ya kuaminika kwa njia na taratibu za kufuata Njia na taratibu za kufuata Njia Bora; na moyo wake wa maringo, na usio na uvumilivu ana mashaka juu ya uaminifu wa wale wanaoelewa na kufuata mafundisho ya Buddha.

Kwa hakika hakuna kitu kibaya sana kama mashaka. Mashaka huwatenganisha watu. Ni sumu inayobomoa urafiki na kuvunja mahusiano mema. Ni mwiba unaochoma na kuumiza; ni sime inayoua.

Vianzo vya imani tangu zamani vilipandikizwa kwa huruma ya Buddha. Mtu anapopata imani yampasa atambue ukweli huo na amshukuru Buddha kwa wema wake.

Mtu inabidi asisahau kuwa siyo kwa sababu ya huruma yake

ambayo imeamsha imani, ila kwa sababu ya huruma ya Buddha ambayo kwa muda mrefu imeongeza mwanga wake mtakatifu katika mioyo ya binadamu na kufukuzia mbali giza la ujinga wao. Yule afurahiaye imani ya sasa ameingia katika urithi wao.

Mtu anaweza kuzaliwa katika Nchi Takatifu hata kama anaishi maisha ya kawaida ikiwa ameamsha imani katika huruma ya kudumu ya Buddha.

Kwa hakika, ni vigumu kuzaliwa katika dunia hii. Ni vigumu kuisikia Dharma, ni vigumu zaidi kuamsha imani, kwa hiyo kila mmoja lazima ajaribu kwa kadri awezavyo kuyasikiliza mafundisho ya Buddha .

## IV
## METHALI TAKATIFU

1. " Alinitukana, alinicheka, alinipiga. "Hivyo ndivyo mtu anavyofikiria na kwa kuwa anaendelea kushikiria mawazo ya namna hiyo hasira yake huendelea kupanda.

Hasira haiwezi kuisha ikiwa kuna mawazo ya chuki katika moyo. Hasira itakwisha mara tu mawazo ya chuki yatakapo sahaulika. Kama paa ya nyumba imetengenezwa vibaya mvua itapenyeza hadi ndani; hivyo choyo hupenya ndani ya moyo ambao haukufunzwa vizuri.

Kuwa mvivu ni barabara fupi ya kuelekea kifoni na kuwa na bidii ni njia ya uzima; watu wajinga ni wavivu, watu wenye busara ni watendaji.

Mtengenezaji wa mishale hujitahidi kutengeneza mishale iliyonyooka vilevile mtu mwenye busara huweka moyo wake kwa unyoofu.

Moyo usumbukao hautulii kamwe; hurukaruka hapa na pale na ni vigumu kuutawala, lakini moyo wa starehe ni mtulivu; kwa hiyo ni busara kuutawala moyo.

Ni moyo wa mtu mwenyewe na wala siyo wa adui yake unaomshawishi mtu kumwelekeza kwenye njia za maovu.

Mtu auzuiaye moyo wake kutokana na choyo, hasira na ujinga ni yule aifurahiaye amani ya kweli na ya kudumu.

2. Kusema maneno mazuri bila ya kuonyesha matendo ni kama ua zuri lisilo na manukato.

Harufu nzuri ya ua haielei kupingana na upepo; lakini hasira ya mtu mwema huenda ikipingana na upepo katika dunia.

Usiku huonekana mrefu kwa mtu asiye na usingizi na safari huonekana ndefu kwa msafiri aliyechoka; kwa hiyo muda wa madanganyo na mateso huonekana mrefu kwa mtu asiyejua mafundisho sahihi.

**Njia ya kufaidika kwa vitendo**

Mtu awapo safarini yampasa kusafiri na rafiki yake mwenye moyo sawa na wake au mwenye moyo bora zaidi; heri mtu asafiriye peke yake kuliko kusafiri na mjinga.

Rafiki mwovu na asiye mwaminifu ni wa kuogofya kuliko mnyama pori. Mnyama pori anaweza kujeruhi mwili wako, lakini rafiki ataujeruhi moyo wako.

Ikiwa mtu hawezi kuutawala moyo wake ataridhikaje kwa kufikiria mawazo kama, " Huyu ni mwanangu" au " Hii ni hazina yangu?" Mtu mjinga huteswa na mawazo kama hayo.

Kuwa mjinga na mtu kutambua kuwa ni mjinga, ni bora kuliko kuwa kuwa mjinga na mtu kufikiria kuwa ana busara.

Kijiko hakiwezi kuwa na mwonjo wa chakula kinachokibeba. Hivyo, mjinga hawezi kuelewa hekima ya mtu mwenye busara hata kama atajihusisha na mtu mwenye hekima.

Maziwa mabichi hayagandi kwa urahisi, hivyo matendo maovu hayaleti matunda ya moja kwa moja. Matendo maovu ni kama makaa ya moto yaliyofichwa katika majivu na yakaendelea kufuka moshi na mwisho kutokea moto mkali.

Ni ujinga kwa mtu kutamani mapendeleo, kupandishwa cheo, faida au heshima kwa sababu tamaa kama hizo haziwezi kuleta furaha bali zitaleta mateso.

Rafiki mwema anayetangaza makosa na upungufu wa watu na kukemea maovu anapaswa kuheshimiwa kana kwamba amefichua siri ya hazina iliyofichwa.

3. Mtu anayefurahi anapopewa mafundisho mazuri atalala kwa amani, kwani kutokana nayo moyo wake umetakasika.

Fundi Seremala hujitahidi kunyosha mihimili yake; mtengeneza mishale hujitahidi kuitengeneza vizuri; mchimbaji mtalo wa maji hujitahidi kuutawala moyo wake ili ukafanye kazi kwa ufasaha na kweli.

Mwamba mkubwa hausumbuliwi na upepo; moyo wa mtu mwenye busara hausumbuliwi na heshima au bezo.

Kuiteka nafsi ni ushindi mkubwa kuliko kuteka maelfu ya watu katika uwanja wa vita.

Kuishi siku moja na kupokea mafundisho mazuri ni bora kuliko kuishi miaka mia moja bila ya kuyajua mafundisho hayo.

Wale wanaojiheshimu yawapasa kujichunga wasije wakaanguka tena katika tamaa mbaya. Katika wakati mmojawapo wa maisha yao; katika ujana, utu uzima au uzeeni yawapasa kuamsha imani zao.

Dunia daima inawaka moto, inawaka moto wa uchoyo, hasira na ujinga; mtu yeyote yule anapaswa kuwa huru kutokana na hatari hizi mapema iwezekanavyo.

Dunia ni kama povu, ni kama matando ya buibui, ni kama najisi katika mtungi mchafu; yampasa mtu kujitahidi kila mara kulinda utakatifu wa moyo wake.

4. Kiini na asili ya mafundisho ya Buddha ni; kuepuka ubaya wowote, kutafuta wema, na kutunza moyo katika utakatifu; hiki ni kiini cha mafundisho ya Buddha.

Uvumilivu ni mojawapo kati ya taratibu ngumu lakini ni yule yule mvumilivu atakayepata ushindi.

Ni vema mtu kuondoa chuki anapojisikia kuchukizwa; ni vema kuondoa masikitiko anaposongwa na masikitiko; ni vema kuondoa uchoyo anapozama katika uchoyo. Ili kuishi maisha yasiyo na uchoyo yampasa mtu asijihesabie lolote katika mali yake.

Kuwa na afya njema ni faida kubwa; kutosheka na kile mtu alichonacho ni bora kuliko kuwa na utajiri mkubwa, kuwa wa kuaminika ni alama ya kweli ya urafiki; kuupata Wongofu ni furaha ya hali ya juu.

Wakati mtu ana hisia ya kuchukia maovu, wakati mtu anajisikia huru, wakati mtu anaona furaha ya kusikiliza mafundisho mema, wakati mtu ana hisia hizi na kuzithamini, yeye hana woga tena.

Usifungamane na mambo uyapendayo; usiepukane na mambo uyachukiayo. Huzuni, woga na kufungamana vyote

hutokana na yale mtu anayoyapenda na asiyoyapenda.

5. Kutu inayoharibu chuma huota kwenye chuma chenyewe; vivyo hivyo ubaya huota ndani ya moyo wa binadamu na kumharibu.

Maandiko matakatifu yasiyosomwa kwa uaminifu hayakawii kufunikwa na vumbi; nyumba isiyopata ukarabati wakati inahitaji matengenezo itaharibika na kuchafuka; vivyo hivyo mtu mvivu hakawii kunajisika.

Matendo mabaya humnajisi mtu; ubahili hunajisi matoleo; kwa hiyo matendo maovu hunajisi siyo tu maisha ya sasa bali hata maisha yajayo.

Lakini najisi iliyo mbaya zaidi ni najisi inayotokana na ujinga. Binadamu hawezi kutumaini kutakatisha mwili wake au moyo wake hadi atakapoondokana na ujinga.

Ni rahisi kuangukia kwenye upungufu, kuwa fadhili na jasiri kama kunguru, kuwaumiza watu wengine bila kuwa na fikra ya majuto.

Ni vigumu mno mtu kuwa mnyenyekevu, kuijua heshima na tahadhima, kuepukana na mapendo, kuwa mtakatifu katika mawazo na matendo na kuwa na busara.

Ni rahisi kuyaona matendo ya watu wengine bali ni

vigumu kukubali makosa yako. Binadamu hutangaza madhambi ya watu wengine bila kujali, lakini huficha dhambi zake kama mcheza kamali anavyoficha dadu yake ya ziada.

Anga haionyeshi nyayo za ndege, moshi au dhoruba; Mafundisho maovu hayana Uongofu ndani yake; hakuna kitu chochote katika ulimwengu huu ambacho ni imara; bali moyo wa Uongofu hauteteleki.

6. Kama askari alindavyo lango la ngome yake, ndivyo mtu impasavyo kulinda moyo wake kutokana na hatari za ndani na hatari za nje; mtu asisahau hilo hata kidogo.

Kila mtu anajitawala; ni chemichemi anayoweza kutegemea; kwa hiyo kila mmoja ajitawale mwenyewe.

Hatua za kwanza kuelekea kwenye uhuru wa kiroho kutoka kwenye pingu na vifungu vya dunia ni kutawala moyo, kuacha maneno yasiyo na maana na kuwa na mawazo ya kadri.

Jua huangaza, mchana mbalamwezi huufanya usiku upendeze, nidhamu hukuza heshima ya mpiganaji hivyo kutabaruku kimya kimya hubainisha mtafutaji wa Nuru/ Uongofu.

Yule asiyeweza kulinda na kutawala milango mitano ya fahamu za macho, masikio, pua, ulimi na mwili, na anajaribiwa na mazingira yake si mmojawapo wa watu wanaoweza kujifunza

kuushika Uongofu. Yule anayechunga vizuri malango ya njia kuu za fahamu na kuutawala moyo wake ndiye atakayefaulu kushika Nuru.

7. Mtu anayeshawishiwa na mapenzi yake na machukizo yake hawezi kuelewa kwa ufasaha umuhimu wa neema na huelekea kutekwa; yule asiyetawaliwa na mapendo anaelewa kwa uhakika neema na kwake vitu vyote vinakuwa vipya na vya maana.

Furaha hufuatwa na huzuni, huzuni hufuatwa na furaha lakini mtu anaposhindwa kutofautisha furaha na huzuni, tendo bora na tendo baya huyo ana uwezo wa kuupata uhuru.

Kuwa na wasiwasi katika matumaini au kuyahifadhi masikitiko ya wakati uliopita ni sawa na matete yaliyokatwa na kunyauka.

Siri ya afya ya mwili na moyo siyo ya kuomboleza kwa ajili ya nyakati zilizopita. Siyo kuwa na wasiwasi na mambo ya baadaye au kutarajia matatizo bali kuishi kwa busara na juhudi katika wakati uliopo.

Msihangaikie yaliyopita wala kuota yajayo bali tuliza moyo katika wakati uliopo.

Ni vema kufanya kazi iliyopo sasa kwa ukamilifu bila kushindwa; msihangaike kuikwepa au kuihairisha kazi hiyo hadi kesho. Utaweza kuishi maisha mema leo kwa kutenda sasa.

**Njia ya kufaidika kwa vitendo**

Hekima ni kiongozi bora na imani ni mwenzi mwema. Ni lazima mtu alikimbie giza la ujinga na mateso na autafute mwanga wa U-ongofu.

Ikiwa mwili na moyo wa binadamu vimesimamiwa barabara, yampasa mtu atoe ushuhuda kwa matendo yake maadilifu. Hii ni kazi takatifu. Imani ndipo itakapokuwa utajiri wake, ukweli utayapa ladha nzuri maisha yake, na kukusanya maadili litakuwa jukumu lake takatifu.

Katika safari ya maisha imani ni chakula, matendo ya uadilifu ni hifadhi, hekima ni mwanga wa mchana na uangalifu wa kweli ni kinga wakati wa usiku. Mtu akiishi maisha matakatifu hawezi kuharibiwa na kitu chochote; ikiwa ameuteka uchoyo uhuru wake hauwezi kuwa na kizuizi cho chote.

Yampasa mtu kusahau nafsi yake kwa ajili ya familia yake; yampasa mtu kusahau familia yake kwa ajili ya kijiji chake; yampasa mtu kusahau kijiji chake kwa ajili ya taifa; na yampasa mtu kusahau kila kitu kwa ajili ya Uongofu.

Kila kitu hubadilika, kila kitu huwepo na kutoweka; hakuna amani na kikomo hadi mtu avukapo mipaka ya maumivu makali ya maisha na kifo.